

**ULINGANISHI WA KIFONOLOJIA KATI YA LAHAJA YA
KIMAKUNDUCHI NA KITUMBATU**

HAFSA MAKAME SALUM

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA MASHARTI
YA KUPATIWA SHAHADA YA UZAMILI M.A KISWAHILI YA
CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2018

ITHIBATI

Aliyetia saini hapo chini anathibitisha kuwa amesoma tasnifu hii itwayo: “**Ulingenishi na Tofauti za Kifonolojia Kati ya Lahaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu**”, na ameridhika kwamba imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuhudhurishwa kwa utahini wa shahada ya uzamili (M.A. Kiswahili) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....

Dkt. Hanna Simpassa

(Msimamizi)

.....

Tarehe

HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile ya Tasnifu hii kama kutoa sehemu ndogo ya tasnifu hii, kielektroniki au njia nyegine yoyote ile bila ya idhini ya Muandishi wa Tasnifu hii au kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

IKIRARI

Mimi, Hafsa Makame Salum, ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu asili na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine ndani na nje ya nchi, kwa ajili ya kutunukiwa shahada inayofanana na hii au nyingine yoyote.

.....

Saini

.....

Tarehe

TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa wazazi wangu wapendwa bwana Makame Salum Nassor, mama Okotani Haji Mussa pamoja na mtoto wangu mpenzi, Ibrahim Mussa Mgasho. Lengo la kuwatunuku kazi hii kuifanya kuwa ni chachu ya kujitoa muhang'a katika mchakato mgumu na weny'e vikwazo vingi ambao wakati wa kutafuta elimu. Hakika elimu ni rasilimali isiyofilisika na isiyoshuka thamani katu abadan.

SHUKRANI

Kwanza ni wajibu wangu kumshukuru Allah (S.W) Muumba mbingu, ardhi na vyote vilivyomo ndani yake. Yeye ndiye aliyeniumba na kunipa mfumo wa maisha, kunijaaliya uzima, afya pamoja na kunipa maarifa ya kuweza kukamilisha utafiti huu. Pili, natoa shukrani za dhati kwa uongozi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kupitia msimamizi wangu, Dkt. Hanna Simpassa, ambaye alijitolea kuniongoza na kunisimamia kwa kunipa mawazo, fikra, pamoja na mwongozo wake na ndio ulionisaidia na kunipa msukumo wa kufanya kazi hii hadi kufikia kiwango hiki nilichofikia.

Tatu, napenda kumshukuru mume wangu mpenzi, Bw. Mussa Mgasho Mussa, kwa kunivumilia, kunipa moyo na kuitunza familia yetu vizuri katika kipindi kigumu cha masomo mpaka kukamilisha utafiti huu. Pamoja na mwanangu, Ibrahim Mussa Mgasho, kwa kuvumilia na kukosa rubaa ya mama yake kwa kipindi chote cha masomo.

Pia, nawashukuru wanafunzi wenzangu wote wa shahada ya Uzamili kwa ushirikiano wao kwa muda wote wa masomo, pamoja na wale wote walionisaidia kazi hii na kunipa moyo kwa hali moja au nyingine hadi kukamilika kwake. Wote kwa pamoja nawatachia kila la kheri katika maisha na namuomba Mwenyezi Mungu awalipe malipo mema kutohana na wema wao. Pia kwa amba tulishauriana kila hatua za tafiti zetu, wakiwemo Sabrina Issa Seif, Salma Ahamada Ali, Abdallah Juma, na wengineo. Wengine walionisaidia ni mwalimu Hassan Mussa wa skuli ya sekondari Makunduchi, mwalimu Haji Daru Ukasha na bwana Abdi Ali Kombo. Shukrani zaidi

ziende kwa wale waliochaguliwa kuwa sampuli ya utafiti huu na wakakubali kujaza dodoso bila pingamizi, wakajibu maswali ya usaili bila ya shida na wala vikwanzo vyovyyote. Sina cha kuwalipa, ila ni kuwaombea dua kwa Mungu, awalipe kheri duniani, na kesho akhera. Na bila ya kumsahau Mwalimu Gora Akida Haji aliyeweza kupitia mswada wa kazi hii yote na kuuhariri kabla ya kupelekwa kwa msimamizi.

Mwisho, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitatoa shukurani kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kunipa kibali cha ruhusa ya kufanya utafiti katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar, Vyuo Vikuu pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar. Ninawashukuru wale wote walionisaidia kazi hii kwa hali moja au nyingine bila hata ya kuwataja; na hii si dalili ya kuwadharau hata kidogo kwa mchango wao muhimu katika kazi hii. Msingi wa shukrani hizi ni kuwaombea wote hawa kwa Allah ili awafungulie milango ya kheri na baraka duniani, na kesho akhera.

IKISIRI

Tasnifu hii inachunguza ulinganifu wa kifonolojia kati ya lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi. Utafiti uliofanywa uliongozwa na malengo mahsus matatu ambayo ni: kwanza, Kuchambua mlingano wa matamshi ya fonimu uliopo kati ya lahaja ya Kimakunduchi na lahaja ya Kitumbatu. Pili, Kuchambua tofauti za matamshi ya fonimu zilizopo kati ya lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi. Na tatu ni Kuelezea mambo yaliyosababisha kulingana na kutofautiana kwa matamshi ya fonimu za lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi. Mbinu zilizotumika katika ukusanyaji wa data ni usaili na mahojiano. Nadharia iliyotumika katika utafiti huu wakati wa ukusanyaji na uchambuzi wa data ni nadharia ya Isimu Linganishi na Konsonanti Vokali. Matokeo ya jumla ya utafiti huu yalionesha kuwa kuna mlingano na tofauti za kimatamshi katika fonimu za lahaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu kama zifuatazo: kwa lahaja hizi zimelingana katika vipengele vifuatavyo; kuwa na silabi zenye sifa ya kudondosha fonimu, usilimisho wa matamshi ya fonimu na kuimarisha na kudhofisha matamshi ya fonimu. Pia, Lahaja hizi zimetofautiana katika vipengele vifuatavyo; ukakaishaji wa matamshi ya fonimu, lahaja moja kudhofisha na nyingine kuimarisha matamshi ya fonimu, uyeyushaji wa fonimu kwa lahaja pamoja na tofauti nyingine. Utafiti umebaini kuwa, ulinganifu na utofauti huo unatokana na kuwa ni lahaja zenye asili moja, kuwepo katika kundi moja la lahaja na wanajamii wake kuwa na nyanja za aina moja kiuchumi. Kutokana na matokeo haya, utafiti huu unapendekeza mambo yafuatayo: kwanza ni kutafiti juu ya athari za sayansi na teknolojia katika lahaja za Kiswahili. Pili, kutafiti juu ya mabadiliko ya kifonolojia katika lahaja za kiswahili, kwa kulinganisha miaka ya zamani na hali ya sasa ya lahaja hizo.

YALIYOMO

ITHIBATI.....	ii
HAKIMILIKI.....	iii
IKIRARI	iv
TABARUKU.....	v
SHUKRANI	vi
IKISIRI	viii
ORODHA YA MAJEDWALI	xiii
ORODHA YA VIAMBATANISHO.....	xiv
ORODHA YA VIFUPISHO.....	xv
SURA YA KWANZA	1
UTANGULIZI WA JUMLA.....	1
1.1 Utangulizi	1
1.2 Usuli wa Mada	1
1.3 Tamko la Utafiti	4
1.4 Malengo ya Utafiti	5
1.4.1 Lengo Kuu.....	5
1.4.2 Malengo Mahsus.....	5
1.5 Maswali ya Utafiti	6
1.6 Umuhimu wa Utafiti	6
1.7 Mipaka ya Kitaaluma na Mawanda ya Utafiti	7
SURA YA PILI.....	11
MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUZI CHA NADHARIA	11
2.1 Utangulizi	11

2.2	Dhana na Uchambuzi wa Lahaja za Kiswahili	11
2.3	Dhana ya Fonolojia ya Kiswahili	19
2.3.1	Dhana na Uchambuzi wa Fonolojia	21
2.4	Lahaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu	29
2.5	Nadharia Zilizotumika Katika Kukusanya na Kuchambua Data za Utafiti ...	33
2.6	Pengo la Utafiti	37
	SURA YA TATU.....	38
	MBINU NA NJIA ZA UTAFITI	38
3.1	Utangulizi	38
3.2	Eneo la Utafiti	38
3.3	Walengwa wa Utafiti.....	40
3.4	Jamii ya Watafitiwa.....	40
3.5	Sampuli na Usampulishaji.....	40
3.5.1	Sampuli Lengwa.....	41
3.6	Mbinu za Kukusanya Data	43
3.6.1	Hojaji.....	43
3.6.2	Mahojiano/Usaili	45
3.7	Vifaa na Zana za Kukusanya Data	46
3.8	Mkabala wa Kuchambua na Kufafanua Data.....	47
	SURA YA NNE	48
	UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA.....	48
4.1	Utangulizi	48
4.2	Uwasilishaji wa Msamiati wa Lahaja ya Kitumbatu na Lahaja ya Kimakunduchi	48

4.3	Ulingenifu wa Fonimu za Lahaja ya Kimakunduchi na ya Kitumbatu.....	51
4.3.1	Kuwa na Tabia ya Kudondosha Fonimu	51
4.3.2	Usilimisho	52
4.3.3	Kuimarisha na Kudhoofisha Fonimu	53
4.3.3.1	Kuimarisha Fonimu	53
4.3.3.2	Kudhoofika kwa fonimu	54
4.4	Tofauti za Fonimu kati ya Lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi	55
4.4.1	Ukakaishaji.....	56
4.4.2	Kuimarika na Kudhoofika kwa Matamshi ya Fonimu	57
4.4.3	Uyeyushaji.....	59
4.4.4	Tofauti Nyingine	59
4.5	Sababu za Kulingana na Kutofautiana kwa Lahaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu.....	61
4.5.1	Sababu za Kulingana.....	61
4.5.1.1	Zinalingana Kwa sababu ya Kutoka Katika Asili ya Lugha Moja.....	61
4.5.1.2	Kuwa katika Kundi (Kanda) Moja ya Lahaja za Kiswahili	62
4.5.1.3	Kufanana kwa Nyanja za Kiuchumi na Kiutamaduni/Kijiografia	63
4.5.2	Sababu za Kutofautiana.....	64
4.5.2.1	Umbali wa Kijiografia.....	64
4.5.2.2	Maingiliano ya Kijamii	65
4.5.2.3	Kuathiriwa zaidi na Kiswahili Sanifu	65
4.5.2.5	Kiwango cha Jamii Kuathiriwa na Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia	66
4.6	Hitimisho.....	67

SURA YA TANO	69
MUHUTASARI WA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	69
5.1 Utangulizi.....	69
5.2 Muhutasari wa Matokeo ya Utafiti	69
5.3 Mapendekezo ya Tasnifu hii	71
5.3.1 Mambo Yakuboreshwa Zaidi Katika Lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi	71
5.3.2 Mapendekezo ya Tafiti za Baadae	72
5.4 Hitimisho.....	73
MAREJELEO	74
VIAMBATANISHO	78

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 3.1: Mgawanyo wa Sampuli Iliyotumika katika Utafiti Huu.....	43
Jedwali Na. 4.1: Msamiati wa Lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi Uliokusanywa kwa Lengo la Kuchambuliwa Kufanana na Kutofautiana kwake	49
Jedwali Na. 4.2: Ulingenifu wa Fonimu za Lahaja ya Kitumbatu na Lahaja ya Kimakunduchi	51
Jedwali Na. 4.3: Tofauti za Fonimu za Lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi	55

ORODHA YA VIAMBATANISHO

Kiambatanisho Na. 1: Muongozo wa Hojaji, Usaili na Ushuhudiaji.....	78
Kiambatanisho Na. 2: Matukio Mbalimbali ya Kiutafiti Kupitia Picha	83

ORODHA YA VIFUPISHO

BAKIZA	Baraza la Kiswahili la Zanzibar
KKAM	Kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki
Km	Kimakunduchi
Ks	Kiswahili Sanifu
Kt	Kitumbatu
n.k	Na kadhalika
TUKI	Taasisi ya Uchunguzi ya Kiswahili

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Utangulizi

Sura hii inajadili masuali ya kiutangulizi kuhusu juu ya kulingana na kutofautiana kifonolojia kati ya lahaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu. Sehemu hii imeeleza usuli wa mada ya utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mipaka ya utafiti huu.

1.2 Usuli wa Mada

Lugha ya Kiswahili imekuwa na historia ndefu na yenyewe utatanishi baina ya wataalamu. Vilevile kumekuwa na mabishano dhahiri ya kitaaluma hasa katika kuangalia chimbuko na asili ya lugha ya Kiswahili. Kuna madai mengi ambayo yametolewa juu ya asili ya Kiswahili, kama vile Kiswahili ni kibantu, Kiswahili ni kiarabu, Kiswahili ni Kikongo, Kiswahili ni lugha chotara na kadhalika. Massamba na wenzie (2001) wanaeleza kuwa, Zimewahi kutolewa nadharia tete kadhaa kuhusu asili ya lugha ya Kiswahili, lakini zilizo muhimu ni nne. Nadharia tete ya kwanza, ingawa si kwa ubora, ni ile isemayo kwamba Kiswahili kimetokana na lugha ya Kiarabu; ya pili ni ile isemayo kuwa Kiswahili kimetokana na mchanganyiko wa lugha ya Kiarabu na lugha za kibantu zilizokuwa katika upwa wa Afrika Mashariki; ya tatu inasema kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu iliyoathiriwa sana na lugha ya Kiarabu; na ya nne inadai kwamba lugha ya Kiswahili ni mchanganyiko wa lugha kadhaa za Kibantu zilizokuwa katika upwa wa Afrika Mashariki na kuathiriwa sana na Kiarabu, katika kipengele cha msamiati katika kukua kwake. Dondoo hii imethibitisha uwepo wa uchangamano katika suala la asili ya lugha ya Kiswahili.

Pia, wapi kimeanza Kiswahili ni dhana tatanishi ila wengi wa wataalamu na watafiti wa zamani wanaeleza kuwa chimbuko la lugha ya Kiswahili ni maeneo ya Kaskazini mashariki ya Kenya kama vile maeneo ya Pate, Lamu na kadhalika.

Nadharia hii inaeleza kuwa Kiswahili kilichimbukia Kenya na kuenea katika mwambao wa Afrika Mashariki hatua kwa hatua. Kama vile kuingia pwani ya Mombasa, Tanga, Zanzibar na kuelekea maeneo ya Bagamoyo, Kilwa hadi Msumbiji. Hoja hii haikufunga mjadala kama anavyoeleza Masebo na Nyangwine, (2002), kuwa; suala la mahali hasa ambapo ndiyo chimbuko la lugha ya Kiswahili wataalam wanahitafiana. Wengine wanadai kuwa lugha ya Kiswahili inatokana na Kingozi, lugha ya Kaskazini Mashariki mwa Kenya, na wengine wamesema kuwa Kiswahili chimbuko lake ni Kichomvi kilichozungumzwa na watu wa Bagamoyo, Mzizima; eneo linalojulikana kwa jina la Dar es Salaam hadi Kilwa. Kwa jumla, madai ya wataalam hawa hayajawahi kuthibitishwa na mtu ye yote kwa hoja makini. Dondoo hii nayo imethibisha mvutano uliopo juu ya suala la chimbuko la lugha ya Kiswahili.

Kwa upande wa wanahistoria kama Sharifu, (1982) na wengine wao wanaeleza juu ya chimbuko la watu wa pwani hususani watu wa Zanzibar, wapo wanaoeleza kuwa watu wa Zanzibar walitokea maeneo ya Kaskazini Mashariki mwa Kenya wakitokea Uajemi kwa kutumia madau na mitumbwi ya matanga kwa kutumia pepo za kusi na kaskazi. Watu hawa walifika Unguja kupitia kisiwa cha Tumbatu na kuwaacha watu ambaao baadae wakajenga makaazi na kutumia lahaja ya Kitumbatu na wengine wa kaendelea na msafara hadi maeneo ya Malindi na kuwaacha watu wakiishi na kujenga makazi na kutumia lahaja ya Kiunguja mjini. Na wengine kufika Makunduchi maeneo ya Nganani, hawa waliishi hapo na baadae kutumia lahaja ya Kimakunduchi. Pia,

kuna wale waliopitia kisiwa cha Pemba moja kwa moja na kuishi huko baadae kutumia lahaja ya Kipemba.

Lahaja hizi zimeibuka kutokana na watu hawa kutofautiana kimazingira, kiuchumi na kiutamaduni baina ya jamii hizo. Pamoja na kupata mchanganyiko wa watu wengine kutoka katika maeneo ya bara za juu, watu waliokuja kwa shughuli za kiuchumi, bara la Asia, Amerika na kadhalika.

Kihistoria kumekuwa na uhusiano mkubwa kidamu kati ya Watumbatu na Wamakunduchi, Sharif (keshatajwa). Uhusiano huu, pia upo hasa katika suala la kilugha na utamaduni kwa jumla. Lahaja ya Kitumbatu pamoja na kutengwa na Kimakunduchi kwa kugawiwa kati kati na Kiswahili sanifu imekuwa na ukaribu zaidi na lahaja ya Kimakunduchi katika kipengele cha msamiati, kifonolojia, kimofolojia na hata kisemantiki.

Nguvu za uhusiano huu huenda ikawa inapungua hatua kwa hatua kutokana na Kiswahili sanifu kuwa karibu zaidi kijiografia na lahaja ya Kitumbatu kwa upande mmoja na kuwa karibu na lahaja ya Kimakunduchi kwa upande wa pili. Kwa ujumla, Zanzibar ina lahaja kuu nne, ambazo ni lahaja ya Kiunguja mjini ambayo hivi sasa ni (Kiswahili sanifu) inayozungumzwa mjini na Magharibi, lahaja ya Kitumbatu, ambayo inazungumzwa kaskazini mwa kisiwa cha Unguja, lahaja ya Kimakunduchi au Kihadimu kama baadhi ya wataalamu wanavyokiita, ambayo inazungumzwa kusini mwa kisiwa cha Unguja. Na lahaja ya Kipemba ambayo inazungumzwa kisiwa cha Pemba.

Lahaja ya Kitumbatu imekuwa na uhusiano wa karibu kimsamiati, kimatamshi na hata kisemantiki na lahaja ya Kimakunduchi, kuliko lahaja ya Kipemba. Hivyo huenda lahaja hizi zikalingana zaidi kifonolojia, pia kuwepo na tofauti za hapa na pale kutokana na kutenganishwa na lahaja ya Kiunguja mjini (Kiswahili sanifu).

1.3 Tamko la Utafiti

Mazingira ya kitamaduni yamethibitisha uhusiano wa watu wa Tumbatu na Makunduchi, kwa kuonesha kuwa ni watu wenye asili na chimbuko la lugha moja. Jamii zote zimekuwa na utamaduni wa aina moja kama vile utamaduni wa Kuoga Mwaka kwa wakati tena kwa mawasiliano ya karibu katika kuratibu siku ya kuoga. Kwa upande wa lugha, Zanzibar ni sehemu ndogo katika nchi za Afrika ya Mashariki ila ni sehemu yenye lahaja nyingi zaidi katika lahaja za Kiswahili. Zanzibar ina jumla ya lahaja nne: lahaja ya Kitumbatu, lahaja ya Kimakunduchi, lahaja ya Kipemba na lahaja ya Kiunguja Mjini. Tafiti nyingi zimefanyika kwa kuangalia lahaja ya Kitumbatu na Kimakuduchi kama vile, Hill (1973) alifanya utafiti katika lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi kwa kuangalia sauti zilizomo katika lahaja hizi. Makame (2016), kachunguza muundo wa virai nomino katika lahaja ya Kitumbatu. Wakati Bavuai (2015), alichunguza muundo wa Kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi.

Bakari (2015) alichunguza ulinganishi wa kiisimu kati ya lahaja ya Kipemba na lahaja ya Kitumbatu. Saleh (2013), aliangalia athari za kiisimu kwa lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu kinachotumika Shulen Makunduchi Zanzibar. Wataalamu hawa kwa kiasi wamejumuisha kuwa Lahaja ya Kimakunduchi na lahaja ya Kitumbatu zina matamshi ya aina moja, hasa katika maneno ambayo katika Kiswahili sanifu yamesanifiwa na kurahisishwa matamshi hayo. Mfano maneno kama kula,

kulala, muume n.k. Pia lahaja hizi zimekuwa zikitofautiana kwa maneno fulani juu ya matamshi ya maneno hayo. Pia, baadhi ya maeneo ya Kusini Unguja yameanza kupoteza hadhi ya kuzungumza lahaja ya Kimakunduchi, kutokana na sababu mbalimbli ikiwemo ya kuwa karibu sana na kuathiriwa na Kiswahili sanifu.

Hivyo basi, mtafiti pamoja na jitihada yote ya kusoma hakuona au kusikia tafiti zinazozungumzia kuhusu kulingana na kutofautiana kifonolojia kati ya lahaja ya Kimakunduchi na lahaja ya Kitumbatu. Kwa hiyo akaona ipo haja ya kuziba pengo lililoainishwa hapo juu kwa kuchunguza kulingana na kutofautiana kifonolojia kati ya lahaja ya kimakunduchi na lahaja ya kitumbatu.

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu umekuwa na malengo ya aina mbili, lengo kuu na malengo mahsus; malengo haya yalikuwa ndio muongozo wa utafiti huu.

1.4.1 Lengo Kuu

Kuchunguza ulinganifu na tofauti za kifonolojia kati ya lahaja ya Kimakunduchi na lahaja ya Kitumbatu.

1.4.2 Malengo Mahsus

Utafiti huu uliongozwa na malengo mahsus yafuatayo;

- (i) Kuchambua mlingano wa matamshi ya fonimu uliopo kati ya lahaja ya Kitumbatu na ya Kimakunduchi.
- (ii) Kuchambua tofauti za matamshi ya fonimu zilizopo kati ya lahaja ya Kimakunduchi na ya Kitumbatu.

- (iii) Kuelezea mambo yanayosababisha kufanana na kutofautiana katika matamshi ya fonimu kati ya lahaja ya Kimakunduchi na ya Kitumbatu.

1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulitumia maswali badala ya mabunio, na uliongozwa na maswali ya utafiti yafuatayo,

- (i) Je, kuna mlingano gani wa sauti kati ya lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi?
- (ii) Je, kuna tofauti gani za sauti kati ya lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi?
- (iii) Ni mambo gani yanayosababisha kufanana na kutofautiana kisauti kati ya lahaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Baada ya kukamilika kwake, utafiti huu utasaidia watu wa makundi mbalimbali; kwanza wanajamii kwa kujua namna lahaja ya Kitumbatu na Kimakundichi zinavyotofautiana na kulingana kifonolojia. Kwa lengo la kuona uhusiano dhahiri wa lugha hizi. Pili, kwa wanataaluma, utafiti huu utakuwa mchango mkubwa katika taaluma ya isimu- historia na isimu – linganishi katika lahaja za Kiswahili. Kwa kujua lahaja za Kiswahili zinalinganaje na zinatofautianaje kiisimu. Pia matokeo ya utafiti huu yatasaidia kuchambua sababu zilizosababisha kutokea kwa mlingano na tofauti kati ya lahaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu, ikiwa kiisimu, kimazingira ua hata kimuktadha. Pia, utafiti huu unatarajiwa kuwa ni rejea kwa walimu na wanafunzi wa kila ngazi, katika maktaba za vyuo na hata shule ili kutumiwa na wasomi pamoja na watafiti wengine katika shughuli zao za kiutafiti.

1.7 Mipaka ya Kitaaluma na Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu umejikita katika kuchunguza ulinganifu na tofauti kwa sauti (matamshi) katika msamiati unaotumika baina ya lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi na nini kinasababisha kulingana na kutofautiana huko. Utafiti umeteua msamiati maalumu ili kuchunguza ulinganfu na tofauti kwa sauti za lahaja hizi mbili. Misamiati ambayo imechunguzwa katika utafiti huu ni ile inayotumika katika lahaja zote mbili kwa maana moja na mazingira ya aina moja kimatumizi kati ya lahaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu. Uchunguzi wa utafiti huu umejikita hasa kuangalia kulingana na kutofautina kifonolojia katika lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi.

1.8 Vikwazo vya Utafiti

Mtafiti alipata vikwanzo mbali mbali ambavyo vingine vilikwa ni changamoto ya kazi hii na vingine vilibakia kuwa ni tatizo kwa utafiti huu. Miongoni mwa vikwanzo hivyo ni:

Madodoso mengi kutokurudi kwa wakati na mengine kutokurudi kabisa. Mtafiti alipata kikwazo cha madodoso yaliyopelekwa kwa watafitiwa hayakurudi kwa wakati. Hali hii ilimchelewesha mtafiti kuweza kuendana na ratiba iliyopangwa katika utafiti huu. Pia, kuna madodoso ambayo hayakurudi kabisa kutoka kwa watafitiwa. Katika kukabiliana na hili mtafiti alitolesha dodoso zaidi na idadi iliyokisiwa katika utafiti huu.

Ugumu wa mazingira ya eneo la utafiti. Mtafiti alipata shida kutokana na eneo lililofanyiwa utafiti huu. Miongoni mwa aneo la utafiti huu ilikuwa ni kisiwa cha Tumbatu, kisiwa ambacho kimekuwa kigumu kwa suala la usafiri na hasa kwa mgeni. Eneo hili linakubidi uvuke bahari kwa viboti au vidau, na wakati mwengine unaweza

kulazimika kulala Tumbatu kwa kukosa usafiri au kutumia gharama kubwa zaidi ya kukodi kiboti. Katika kukabiliana na hili mtafiti ilibidi kutafuta mwenyeji wa Tumbatu kwa ajili ya kupata hudumu za kula na malazi kwa sababu eneo hili halina nyumba za wageni wala hoteli.

Baadhi ya watafitiwa kutokuwa tayari kutoa data bila ya kulipwa. Baadhi ya watafitiwa hasa wazee walikuwa hawakotayari kutoa mashirikiano na mtafiti hadi pale watakapolipwa. Hali hii ilitokana na imani kuwa taarifa watakazo toa zinaweza kumtajirisha mtafiti na wao wasifaidike na kitu. Katika kubaliana na hili mtafiti alijaribu kuwa elimisha lengo la utafiti huu pamoja na taratibu zake. Wakati mwengine ilimplazimu mtafiti kuachana na mtafitiwa kwa lengo la kuepuka kukiuka maadili ya utafiti.

Maswali katika mbinu ya usaili kutokujibika ipasavyo. Maswali mengi ambayo yaliulizwa kwa sampuli ya wazee yalikuwa na ugumu wa kupata majibu kama ilivyotarajiwa na mtafiti. Wazee wengi walikuwa wakijaribu kueleza historia ya maeneo yao. Hali hii ilimfanya mtafiti kutumia juhudhi ya ziada kuititia sampuli ya wataalamu ili kuziba pengo hilo. Pia, tulijaribu kufatilia wazee waliowahi kusoma hasa katika fani ya uwalimu ili kutusaidia kupata data za utafiti wetu.

Haikuwa rahisi kwa watafitiwa kueleza maneno yaliyomo katika baadhi ya maswali.

Mfano: neno **fonolojia**, ilimfanya mtafiti atumie muda wa zaidi kuwafahamisha mpaka kuelewa. Vilevile baadhi ya watafitiwa lafudhi zao kuanza kupotea kutokana na upotevu wa meno. Hivi ni baadhi ya vikwanzo alivyopambanavyo mtafiti katika kazi yake na namna alivyoweza kukabilana navyo.

1.8 Mpangilio wa Tasnifu

Tasnifu hii imejengeka kwa sura tano zenyе kutegemeana na pia kujitegemea kimaudhui katika mjengeko wake. Kwa ufupi sura hizi zimejumuisha mambo yafuatayo:

Sura ya kwanza; ni sura tangulizi katika tasnifu hii kwa kujumuisha vipengele vinane. Kwanza ni usulu wa mada ya kazi hii. Usuli huu umefafanua juu ya asili na chimbuko la lugha ya Kiswahili pamoja na kufafanua lahaja na uhusiano kati ya lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi. Pili, ni uchambuzi wa tamko la tatizo lililofanyiwa utafiti huu. Tatu, ni malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umihimu wa utafiti, mawanda ya kitaaluma na mipaka ya utafiti, vikwanzo vya utafiti pamoja na kipengele cha mpangilio wa tasnifu hii.

Sura ya pili, imechambua marejeleo mbali mbali yanayohusiana na mada hii. Sura hii imegawiwa sehemu tano; kwanza dhana na uchambuzi wa lahaja. Pili, dhana na uchambuzi wa fonolojia ya Kiswahili. Tatu, tafiti kuhusu lahaja ya Kimakunduchi na lahaja ya Kitumbatu. Nne, ni uchambuzi wa nadharia zilizotumika katika utafiti huu, wakati utafiti huu ulitumia nadharia ya Konsonenti Vokali, na nadharia ya Isimu linganishi. Na mwisho ni mapengo ya mapitio ya kazi tangulizi.

Sura ya tatu, ilichambua mbinu na njia ya ukushanyaji na uchambuzi wa data za tasnifu hii. Sura hii imechambua vipengele mbali mbali navyo ni; eneo la utafiti, walengwe wa utafiti, jamii ya watafitiwa, sampuli na usampulishaji ambapo utafiti wa kazi hii ulitumia sampuli lengwa. Vipengele vingine ni mbinu za kukusanya data, na mbinu zilizotumika ni hojaji na mahojiano, vifaa na zana za kukusanya data pamoja na mbinu za kuchambua na kufafanua data.

Sura ya nne, imebeba mada ya uchambuzi na ufanuzi wa data za utafiti huu. Sura hii imejengwa kwa sehemu nne. Sehemu ya kwanza imejumuisha msamiati wa lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi uliokusanywa katika utafiti kwa lengo la kutumia kulinganisha lahaja hizi kwa kuonesha kulingana na kutofautiana. Sehemu ya pili ni mlingano wa fonimu kati ya lahaja ya Kimakunduchi na lahaja ya Kimakunduchi. Sehemu ya tatu ni tofauti za fonimu kati ya lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi. Na, mwisho ni sababu za kufanana na kutofautiana kati ya lahaja hizi mbili.

Sura ya tano, ni sura ya mwisho ya tasnifu hii. Sura hii imejengeta kwa sehemu kuu tatu. Kwanza, muhtasari wa tasnifu hii. Pili, ni mchango wa tasnifu. Na, mwisho ni hitimisho la jumla ya tasnifu hii.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUZI CHA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Sehemu hii inahusu mapitio ya machapisho na tafiti mbalimbali zilizopata kuzungumzia mada inayofanana au kukaribiana na mada inayofanyiwa utafiti, pamoja na kuainisha nadharia zilizotumika. Tafiti mbalimbali zimesomwa na kupembuliwa. Upembusi huo ulizingatia vipengele vinavyohusu dhana ya lajaja, fonolojia kwa kuzingatia maana, vipengele vya msingi na uchambuzi wake. Tafiti zinazohusu lajaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi pamoja na kubainisha pengo la utafiti lililopatikana kutokana na kazi tangulizi. Malengo makuu ya mapitio haya ni kupata picha ya jumla ni kwa jinsi gani wanaisimu wamezungumzia tofauti na mlingano wa kifonolojia baina ya lugha moja na nyingine na kati ya lajaja moja na nyingine. Taarifa hizo zilimsaidia sana mtarufi kubaini kuwa mawanda ya tofauti na mlingano baina ya lajaja na jinsi yanavyoweza kufanyiwa kazi. Kutokana na mapitio hayo mtarufi alijua pengo linajitokeza na kulifanya utafiti wa kina kuhusu kulingana na kutofautiana kifonolojia kati ya lajaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu ili kuongeza maarifa mapya katika kipengele hiki cha lajaja na lajajia.

2.2 Dhana na Uchambuzi wa Lajaja za Kiswahili

Wataalamu mbali mbali wamefasili dhana ya lajaja kutokana na mitazamo yao tofauti. Baadhi ya wataalamu waliofasili dhana ya lajaja ni TUKI (2004) wanaoleza kuwa; lajaja ni tofauti katika matamshi, maumbo na matumizi ya maneno katika maeneo mbali mbali kwa lugha yenye asili moja. Mkude (1983) anasema kuwa lajaja ni usemaji unaoangukia katikati ya usemaji wa mtu binafsi na usemaji wa jamii ya

wasema lugha moja. Masanjila (2009) anaeleza kuwa Lahaja ni moja wapo kati ya lugha ambazo kimsingi huhesabiwa kuwa ni lugha moja ispokuwa zinatofautiana katika baadhi ya vipengele fulani fulani kama vile lafudhi, fonolojia, msamiati usiokuwa wa msingi au muundo kutokana na eneo lugha inapozungumzwa. Nae Kipacha, (2003) anaeleza kuwa, Lahaja ni matokeo ya lugha kuwa na launi kadhaa zinazowabainisha watumiaji wake mahali watokapo au tabaka lao. Tofauti za launi hizo haziathiri maelewano baina ya mfumo na kanuni ya miundo ya lahaja hizo. Maana hizi zilisaidia utafiti huu kwa kuona kuna vipengele gani vinavyotofautisha lahaja moja na nyingine kama vile matamshi, maumbo na matumizi ya maneno na ndio msingi wa tofauti za lahaja. Katika vipengele hivi utafiti huu ulijikita katika kipengele cha fonolojia ili kuangalia kulingana na kutofautiana kwa lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi.

Wapo wanataaluma wengine kadhaa, wamejaribu kueleza maana ya lahaja kwa njia tofauti tofauti. Kama ilivyokwisha bainishwa hapo juu, mionganoni mwa wanataaluma waliojihuisha na eneo hili ni waandishi wa *Oxford Advanced Learners Dictionary of Current English* (2000), Macmillan na Graw Hill (1993) pamoja na Mgullu (1999). Kwa ujumla wao, wataalamu hawa wana maoni kwamba lahaja ni tofauti katika matamshi, maumbo na matumizi ya maneno katika maeneo mbalimbali kwa lugha yenyе asili moja. Ni mfumo wa lugha unaozungumzwa katika eneo fulani na watu wenye matamshi, sarufi na msamiati unaotofautiana kidogo na wazungumzaji wengine wa lugha hiyohiyo wanaoishi eneo jingine la kijiografia.

Mfumo huo wa uzungumzaji huwa unatofautiana kwa kiasi na mfumo wa lahaja sanifu ya lugha hiyo. Kwa maneno mengine tunaweza kusema kwamba, lahaja ni

namna tofauti tofauti za kuizungumza lugha moja. Aina hizi tofauti za kuizungumza lugha moja huwa haziwazuuii wazungumzaji kuelewana. Kawaida uzungumzaji wa lahaja ya Kitumbatu, uzungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi na uzungumzaji wa lahaja nyingine yoyote ya Kiswahili kama Kipemba, Kimvita n.k. kunauelewano unaotokana na mlingano wa vipengele fulani na pia kuna utofautiano unaojengwa na baadhi ya vipengele hivyo. Utafiti huu uliangalia ni kwa kiasi gani kipengele cha kifonolojia kinatoa mlingano na utofautiano kati ya lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Makunduchi.

Kipacha (hapo juu) akiwanukuu, Allen na Linn (1986), na Faguson Gumperz (1960), katika kuchambua dhaana ya lahaja wameangalia katika mtazamo miwili mikuu; mtazamo pungufu na mtazamo wa uelewano. Kwa upande wa mtazamo pungufu wana madai kwamba lahaja ni kilugha ambacho hakijaandikwa, kilugha ambacho hakina maandishi, kwa ufupi huchukuliwa kuwa lahaja ni *lugha pungufu*. Huu ni mtazamo wa kimapokeo ambao unadhoofisha lahaja na kuikweza lugha. Mtazamo huu kwa ufupi, unaipambanua lahaja na lugha kwa kuangalia kipengele cha ukubwa na umaarufu.

Katika mtazamo huu lugha huonekana kuwa ni kitu kikubwa na chenye hadhi ya hali ya juu, wakati ambapo lahaja huonekana kuwa ni kitu kidogo kisicho hadhi yoyote. Watetezi wa mtazamo huu wanaamini kwamba, lugha ni ile inayotumika katika shughuli rasmi kama vile shughuli na harakati za kielimu, shughuli za kiofisi, uendeshaji wa mambo yanayohusiana na mahakama, n.k. Mtazamo huu unaamini kwamba lahaja ni lugha finyu isiyotumika katika shughuli rasmi. Katika mtazamo huu kigezo cha hadhi na ubora kimekitwa kwa kuzingatia kuwepo au kutokuwepo

maandishi. Kipacha (2003) ameona kwamba kigezo cha kimaandishi si cha msingi hata kidogo kwa kuwa kuna baadhi ya ‘vilugha’ visivyo rasmi kama Kimvita, Kipokomo, na Kiamu viro katika maandishi. Kwa ujumla mtazamo huu uliitukuza na kuikweza lahaja iliyoteuliwa kwa ajili ya mawasiliano rasmi iwe ni ‘lughu’ na zile zisizoteuliwa lakini zinatumika katika vitongoji mbalimbali ziwe ni lugha pungufu. Utafiti huu, uliona kuwa hoja hii ni dhaifu na haina mashiko yoyote kwa sababu lahaja zinazofanyiwa utafiti huu yaani Kitumbatu na Kimakunduchi zimekwisha kuandikwa. Kila moja ya lahaja hizi imekuwa na kamusi zaidi ya moja, zimetumika katika maandishi ya kifasihii na maeneo mengine. Hivyo ni kusema kuwa mtazamo huu haukuzingatiwa katika utafiti huu.

Kwa upande wa Mtazamo wa Uelewano Allen na Linn (1986), Faguson Gumperz (1960) wanaeleza kuwa lahaja ni lugha yoyote iwe imeandikwa au haikuandikwa. Waumini wa mtazamo huu hawajapambanua wala kuweka tofauti yoyote kati ya lugha na lahaja. Kwa maneno mengine, wanaona kwamba lugha ni sawa na lahaja. Mtazamo huu ulilazimisha ieleweke kwamba lahaja ni kama sehemu ya kundi-lahaja ambalo linatambulika katika lugha fulani. Hii ina maana kwamba Kiswahili Sanifu ni lahaja iliyoteuliwa rasmi miongoni mwa kundi-lahaja za Kiswahili kwa shughuli fulani za kimawasiliano kama vile elimu na utawala. Kwa muktadha huu tunaposema lugha ya Kiswahili tuna maana ya mkusanyiko wa kundi-lahaja zote za Kiswahili.

Kuteuliwa kwa Kiswahili Sanifu na kusawazishwa na urasmi, hakumaanishi ubora wake, dhidi ya kundi-lahaja nyingine za Kiswahili, bali usawazishaji huo ni jitihada katika kuweka maelewano baina ya vikundi-lahaja. Hii ina maana kuwa iwapo watu wawili mmoja kutoka jamii **A** na mwengine kutoka jamii **B**, wanataka kuzungumza

lakini hawana maelewano baina yao basi watu hao husemwa kwamba wanazungumza lugha mbili tofauti yaani lugha **A** na lugha **B**. Lakini ikiwa watu hawa hawa, mbali ya kuwepo kwa tofauti katika namna za matamshi, maumbo ya maneno, misamiati na hata baadhi ya maana za maneno, lakini bado wanaelewana, watu hawa husemwa kwamba wanazungumza lugha moja mfano lugha **X**. Kwa muktadha huu, tunaweza kusema lugha **A** na Lugha **B** ni lahaja mbili tofauti za Lugha **X**.

Hivyo kigezo cha kupambanua lugha na lahaja ni kigezo cha uelewano. Utafiti huu, unakubaliana na mtazamo huu kuwa ndio mtazamo sahihi katika kutoa dhana ya lahaja. Kwa kuwa Lugha ya Kiswahili imeundwa na lahaja za lugha hii, na zote zinahadhi sawa. Hata lugha rasmi uhai na kukua kwake kunategemea uhai na kukuwa kwa lahaja hizo za Kiswahili. Lahaja ya Kitumbatu na Lahaja ya Kimakunduchi ni miongoni mwa lahaja zilizojenga Kiswahili sanifu. Misingi hiyo hiyo ya uelewano wake ndio inayojenga mlingano na utofautiano kati ya lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi ambapo utafiti huu umejikita.

Watalamu wa lahaja, wamezigawa lahaja za Kiswahili kwa kuzingatia vigezo kadhaa wa kadha. Lakini kigezo muhimu zaidi ni kile kilichozigawa lahaja kwa kuzingatia ukusini na ukaskazini. Watafiti wa lahaja za Kiswahili Nurse na Hinneshbuch (1993) wameorodhesha lahaja za Kiswahili za kaskazini kama ifuatavyo: Chimwini (Mw), Kitukuu (Tu), Kipate (Pa), Kisiu (Si), Kiamu (Am), Kimvita (Mv), Chifunzi (Fu). Kila lahaja miongoni mwa hizi ina eneo lake la kijiografia ambapo inazungumzwa. Lahaja za kusini kwa mujibu wa mgawanyo huu ni Kimrima, lahaja za visiwani; Kiunguja, Kipemba, Kitumbatu na Kimakunduchi. Lahaja nyingine za kusini ni Kimgao, Kingazija n.k. Mtafiti katika andiko hili anapata kuchukua lahaja ya

Kitumbatu na Kimakunduchi kama zote ni lahaja za kusini hata kama kwa upande wa kisiwa cha Unguja lahaja ya Kitumbatu ni lahaja ya Kaskazini ya kisiwa hicho na lahaja ya Kimakunduchi ni lahaja ya Kusini ya Unguja. Kuwepo kwa kundi moja la mgawo huu kunajenga kuwepo kwa mlingano mionganoni mwa lahaja hizi, na kuwepo kwa lahaja moja kusini ya Unguja na nyingine Kaskazini ya Unguja ni sababu ya kuwepo kwa tofauti ya kifonolojia ya lahaja hizo. Hivyo utafiti huu kwa kutumia natija ya rejea hizo ulikusudia kuangalia mlingano na utofautiano wa lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi.

Guillaume (2004), akiingia ndani zaidi katika mgawanyiko wa lugha unaozungumzwa sehemu moja ya nchi yaani lahaja ya sehemu au kwa watu walio katika kundi maalum la jamii ambayo inatofautiana katika maneno, sarufi au matamshi kutoka katika mifumo mengine ya lugha ile ile. Mfano, lugha ya Kiingereza ina aina nyingi za lahaja, Landon pekee inajumuisha lahaja nyingi kuliko lahaja nyingine za lugha ya Kiingereza. Kimsingi lahaja za Kaskazini na Kusini mwa Uingereza zenyewe zinatafautiana katika matamshi, sarufi na miundo ya maneno.

Hali kama hii inajitokeza katika lahaja za Kiswahili za Tanzania. Mfano Zanzibar ni sehemu ndogo katika nchi za Afrika ya Mashariki ila ni sehemu yenye lahaja nyingi zaidi katika lahaja za Kiswahili. Zanzibar inajumla ya lahaja nne; lahaja ya Kitumbatu, Lahaja ya Kimakunduchi, lahaja ya Kipemba na lahaja ya Ki-Unguja mjini (Kiswahili sanifu). Dondoo hii inaonesha dhahiri umuhimu wa kufanya utafiti ili kujuu ni kwa kiasi gani lahaja hizi zinalingana na kutofautiana hasa kwa kipengele cha msingi ambacho ni cha fonolojia. Utafiti huu, ulichunguza hali hiyo, ya kulingana na

kutofautina kifonolojia ipo kwa kiasi gani kati ya lahaja Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi.

Lahaja huibuka kutokana na sababu tofauti kama anavyoeleza Kipacha, (2003) kuwa sababu zifuatazo zinapelekea kuzuka kwa lahaja. Na kuzuka kwa lahaja mbili tofauti inahusisha kutofautiana kwa matamshi, maana ya msamiati au misamiati yenyewe. Ila kipengele cha msingi katika tofauti hizo ni kipengele cha matamshi kinachotokana na fonolojia ya lugha husika. Sababu ambazo husababisha tofauti za kifonolojia na kuzuka kwa lahaja ni kama hizi;

- (i) Sababu za kijiografia
- (ii) Sababu za kijamii

Anaeleza kuwa katika sababu za kijiografia, wazugumzaji wa lugha huweza kutawanyika katika maeneo tofauti pengine kwa matakwa yao binafsi au hata kutenganishwa na maumbile ya kijiografia mfano, kisiwa, mto au mipaka ya kisiasa n.k. Utengano huu wa kijiografia kuna mambo yanayosababisha wanaozungumza lugha moja kutengana kimahali na kimielekeo. Wakitengana, mawasiliano yao hupungua kwa kuwa mawasiliano yao ni kidogo, matokeo yake kuna uwezekano mkubwa wa kuibuka kwa lahaja. Mabadiliko yatokeayo upande mmoja si lazima yatokee upande mwengine. Mabadilko hayo hutokea kutokana na sababu za kieneo na kipelekea tofauti za kifonolojia, msamiati au miundo ya kisarufi ambayo huwa na tofauti ndogo ndogo. Tofauti hizo huwa ndio chanzo cha kuzuka kwa lahaja na pengine masikizano yakiwa hafifu zaidi baada ya muda husababisha kuzuka kwa lugha nyingine.

Kwa upande wa kijamii, katika sababu za kijamii ambazo husababisha kuibuka kwa lahaja ni kama vile matabaka ya jamii, viwango vya kielimu, kazi, umri, hali ya kiuchumi mazingira ya nyumbani na hata malezi. Kwa kawaida, watu wa kipato cha chini au wenyewe elimu duni hutumia zaidi lugha isiyorasmi, wakati wale wenyewe elimu na kipato cha juu hutumia zaidi lugha rasmi katika mawasiliano. Kwa mfano, nchini China na India kuna lahaja ya tabaka la matajiri na ile ya kimaskini, (Tunu za Kiswahili, 2013a).

Vilevile jambo lingine ambalo linasababisha kuzuka na kuibuka kwa lahaja na namna tofauti za uzungumzaji ni tofauti ya rangi na jinsi, kukiwa na ubaguzi baina ya tabaka au jinsi moja na nyingine husababisha kuwepo kwa vizuizi baina ya matabaka hayo na hiyo huzua tofauti za kilahaja. Kwa mfano, nchini marekani watu weusi wana lahaja yao tofauti na wazungu wenyewe asili ya Marekani. Pia, kuna tofauti za kijamii lugha, hizi ni zile namna za uzungumzaji ambazo hutokana na tofauti za kijamii kama umri, jinsi cheo na hadhi. Kwa mfano, katika kigezo cha jinsi, wanawake hutumia neno *shost* na wanume hutumia neno *msela* wote wakiwa na maana ya rafiki katika Kiswahili sanifu, (Tunu za Kiswahili, 2013b). Dondoo hizi zimechambua kwa kina sababu za kuibuka kwa lahaja, kama vile sababu za Kijografia na za Kijamii, pia zimezungumzia sababu ya kutokea kwa namna tofauti ya uzungumzaji, na namna hii hutokea katika fonolojia (matamshi) na hata katika msamiati kama ilivyoelezwa katika mfano hapo juu. Kwa jumla dondo hizi zilikuwa ni hoja ya kushikiliwa ili kuona ni kwa sababu gani lahaja ya Kitumbatu inalingana na kutofautiana kifonolojia na lahaja ya Kimakunduchi.

2.3 Dhana ya Fonolojia ya Kiswahili

Katika lugha ya Kiswahili kuna mifanyiko na kanuni za kifonolojia. Katika mfanyiko huu, sauti hubadilisha mahali na jinsi ya kutamkwa kwake aghalabu kwa kuhamishwa kutoka eneo moja kutamkwa kwenda nyingine ili kubadili fonimu hiyo. Lugha mbali mbali huwa na ukaakaishaji wa sauti mbali mbali. Mifanyiko ya kifonolojia kuhusu mabadiliko haya hutokea pale ambapo fonimu mbili huambatana katika kuunda vipashio vikubwa kuliko fonimu, yaani: silabi, mofu na maana. Katika hali hii, huweza kuibua mchakato wa mofofonolojia. Mofofonolojia ni taaluma ya isimu ambayo hushughulikia uhusiano baina ya mofolojia na fonolojia. Hatua hii hutilia mkazo sifa za kipashio cha kiisimu, ambacho huathiri viwango vyote viwili vyta kiisimu; mofolojia na fonolojia. Mchakato huu unajumuisha vipengle vyta: - uchopekaji wa irabu, udondoshaji wa irabu, ubadala wa irabu, ufupishaji wa irabu na uimarakaji wa irabu. Vipengele hivi vimetokana na msingi wa nadharia ya Konsonanti Vokali; unaeleza kuwa “kipande ambacho hakina hadhi ya silabi kinahusishwa na silabi kamili” sifa ambayo inabebwa na lahaja zote hizi mbili.

Fonolojia ni tawi la msingi la isimu ya lugha. Fonolojia ni dhana inayoundwa kwa maneno mawili; fono ina maana ya sauti na lojia ni taaluma. Kwa maana hiyo, fonolojia ni taaluma inayoshughulika na uchambuzi wa sauti zinazotumika katika lugha maalumu, kwa kuangalia ala zinazotumika kutamkia sauti, namna zinavyotamkwa na sifa zake. Fonoloji ni taaluma inayoshughulika na jinsi sauti zinavyotumika, zinavyounganishwa na kupangwa katika lugha yoyote mahsusili ili kuunda tungo zenye maana, (Habwe na Karanja, 2007). Pia wanaeleza kuwa sauti hizozinazotumika katika lugha mahsusili hujulikana kama fonimu. Kwa kuwa

fonolojia ni taaluma ya lugha mahsus, utafiti huu umechambua fonolojia ya lugha ya Kiswahili. Ni mahsus kwa kuchambua lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi. Lengo la utafiti ni kuchambua kwa kina juu ya kulingana na kutofautiana kifonolojia kati ya lahaja hizi mbili. Pamoja na kuwa taaluma ya fonolojia ni pana sana. Utafiti huu, ulijikita na kipengele cha msingi cha taaluma hii, ambacho ni vitamkwa. Kihistoria lahaja hizi zimekuwa na ukaribu sana. Ni lahaja zinazozungumzwa na watu waliotoka asili moja na kuwa ni ndugu wa kidamu. Pia, lahaja hizi zimekuwa na tofauti kutokana na kutengwa kijiografia.

Lahaja ya Kitumbatu inazungumzwa Kaskazini mwa Unguja na lahaja ya Kimakunduchi inazungumzwa Kusini mwa Unguja. Katikati ya lahaja hizi zinagawiwa na lahaja ya Kiunguja; lahaja iliyosanifiwa na kuwa ni lahaja rasmi ambayo ni lugha sanifu ya Kiswahili. Kumekuwa na ukaribu hasa na kama sio visawe kati ya istilahi vya vitamkwa, sauti na fonimu. Katika utafiti huu dhana hizi zimeangaliwa kama ni visawe vyenye kueleza dhana ya kuwa ni Visawe ni maneno mawili au zaidi yenye maumbo tofauti lakini yenye uhusiano wa moja kwa moja kimaana, ambapo maneno mawili au zaidi yanaweza kujitokeza katika mazingira yale yale kuwakilisha dhana ile ile. Visawe katika lugha fulani huweza kujitokeza kwa njia mbali mbali ikiwemo ya kusanifisha maneno yenye maana moja kutoka lahaja mbili tofauti. Lahaja hizi zimekuwa na idadi sawa ya fonimu zake kama ilivyo fonimu za lugha ya Kiswahili.

Suala la msingi la kuzingatia wakati wa kupitia kazi hii, na nyinginezo za lahaja ni kuwa ndani ya lahaja moja huundwa na vilahaja zaidi ya kimoja. Vilahaja hivi huweza kutofautiana kimamatamshi na hata kimsamiati. Hii ina maana kuwa watafiti wanaweza

kutafiti lahaja moja ila wakatofautiana katika data zao. Ni vyema katika kuangalia kazi hii, ukazingatia eneo na vilahaja vilivyofanyiwa utafiti huu, kama ilivyoelezwa katika njia na mbinu za utafiti huu.

2.3.1 Dhana na Uchambuzi wa Fonolojia

Massamba, (2001), Fonolojia ni kiwango cha sarufi kinachojishughulisha na uchambuzi wa mfumo wa sauti katika lugha. Yaani ni jinsi ambavyo vitamkwa au sauti za lugha zinavyoungana ili kujenga maneno yanayokubalika katika lugha ile. Kwa maana nyingine fonolojia huhusu utaratibu wa mapangilio wa vitamkwa katika maneno ya lugha. Anaongeza kwa kusema kuwa ingawa lugha mbili au zaidi zinaweza kutumia sauti zile zile, utaratibu wa kuzipanga sauti hizo katika kuumba maneno hauwezi kuwa ule ule.

Matinde, (2012), anaeleza kuwa, fonolojia ni tawi la isimu ambalo wajibu wake ni kuchunguza na kufafanua sauti za lugha na uamilifu wake katika mfumo mahususi. Aliongeza kuwa fonolojia huchunguza katika kuunda vipashio vikubwa zaidi ya fonimu. Mtinde, (katajwa hapo juu) akimnukuu Habwe na Karanja (2004) wanasesma kuwa “Fonolojia ni utanzu wa isimu unaochunguza jinsi sauti za lugha zinavyofanya kazi katika lugha mbalimbali”. Kwa jumla dhanna hizi za fonolojia zilitoa dira ya utafiti huu kwa kuona kuwa katika kuangalia kulingana na kutofautiana kwa lahaja hizi mbili ni kuangalia vitamkwa au sauti za lahaja hizi pamoja na fonimu zake.

Matinde, (juu) alichambua zaidi kuhusu fonolojia kwa kusema kuwa fonolojia imegawika katika matawi mawili:

- (a) Fonolojia vipande; tawi hili huchunguza vitamkwa (sauti) katika lugha husika. Baadhi ya mambo ambayo tawi hili hushughulikia ni pamoja na
 - (i) Uainishaji wa sauti katika lugha fulani (fonimu na alofoni zake)
 - (ii) Ufafanuzi wa sauti hizo kwa kutumia sifa bainifu.
 - (iii) Kueleza jinsi sauti hizo huathiriana zinapokabiliana na sauti zingine katika uundaji wa maneno (mifanyiko ya kifonolojia).

- (b) Fonolojia arudhi; tawi hili huchunguza sifa za kiarudhi ambazo huathiri vipashio vikubwa kuliko fonimu na alofoni zake. Kama vile mkazo, kidato, kiimbo, wakaa na silabi.

Katika matawi haya mawili utafiti huu umejikita katika tawi la kwanza; yaani, fonolojia ya vipande katika kuangalia kulingana na kutofautiana kwa lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi. Na, haukuzingatia tawi la pili la fonolojia, yaani katika kuangalia fonolojia arudhi.

Fonimu ni kipashio cha msingi cha taaluma ya fonolojia. Fonimu ni kipashio kidogo kabisa cha lugha ambacho kina uamilifu wa kutofautisha maana kinapochukua nafasi ya kipashio kingine, maana ya neno asili huweza kubadilika au kupotea. Mfano, Tia, Fia, Lia n.k.

Matinde, (juu) amegawa mitazamo mitatu katika uchambuzi wa fonimu:

- (i) Fonimu kama kipashio cha kisaikolojia
- (ii) Fonimu kama kipashio cha kifonolojia
- (iii) Fonimu kama kipashio cha kifonetiki

Utafiti huu uliangalia fonimu kama kipashio cha kifonolojia, hivyo kipengele hicho tu, ndio kilifafanuliwa katika sehemu hii.

Fonimu kama kipashio cha kifonolojia, mtazamo huu uliasisiwa na wanaisimu wa Prague, husasan Trubetzkoy anayedai kuwa ufasili wa fonimu sharti utokane na uamilifu wa fonimu hiyo ndani ya mfumo wa lugha maalum ambamo fonimu hiyo inatumika. Wanaamini kuwa ili fonimu iwe fonimu katika lugha lazima inapochukua nafasi ya fonimu nyingine maana ya neno la awali sharti ibadilike au ipotee, kama ilivyo katika mifano hiyo hapo juu. Mtazamo huu unatumia vigezo viwili kushadidia msimamo huu.

- (a) Usawazishaji, wanafafanua fonimu kwa misingi ya jukumu la kila fonimu katika mfumo wa kifonolojia. Kipengele hiki wanajiuliza; je, sauti moja yaweza kuwa fonimu moja na wakati mwingine kuwa fonimu nyingine? Mfano katika lugha ya Kidanishi, sauti /t/ inapotokea mwishoni mwa silabi hutamkwa kama sauti /d/ nayo sauti /d/ ikitokea mwishoni mwa silabi hutamkwa kama sauti /ð/, kwa mifano katika maneno:

/hat/ -----hutamkwa-----/had/

/t/-----→/d/

/had/ ----hutamkwa-----/hað/

/t/-----→/ð/

Kutokana na mifano huu, sauti /d/ hujitokeza kama /t/, /d/ na /ð/. Kwa hivyo /d/ ni fonimu moja ambayo hutekeleza majukumu ya sauti zingine. (matinde 2012)

- (a) Usawazishaji changamano, hutokea pale ambapo fonimu mbili tofauti huchukua sifa sawa katika muktadha fulani, hivi kwamba sauti hizo hutamkwa kwa namna

sawa zinapotokea katika mazingira fulani ya kiisimu. Kwa mfano, katika lugha ya Kiingereza, sauti /t/ na /d/ ni fonimu mbili tofauti kimatamshi na sifa za kifonetiki. Mfano:

Bet ----- /betting/ matamshi ya Wamarekani /beriŋ/

Bed ----- /bedding/ matamshi ya Wamerekani /beriŋ/

Katika mazingira haya /t/ na /d/ hutamkwa kama /r/ na wazungumzaji wa Kiingereza hasa sauti hizo zinapotokea katikati ya vokali mbili. Matinde, (keshatajwa).

Kwa jumla mifano hii ilikuwa ni muongozo bora wa utafiti huu, kwa kuona ni namna gani tunaweza kuchambua kulingana na kutofautiana kifonolojia, kati ya lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi kwa kutumia mtazamo wa usawazishaji na usawazishaji changamano.

Katika lugha ya Kiswahili kuna mifanyiko na kanuni za kifonolojia. Katika mifanyiko huu, sauti hubadilisha mahali na jinsi ya kutamkwa kwake aghalabu kwa kuhamishwa kwenye kaakaa gumu kama anavyoeleza Lass (1984). Lugha mbalimbali huwa na ukaakaishaji wa sauti mbalimbali. Wakati, Matinde (hapo juu) Ameeleza kuwa mifanyiko ya kifonolojia kuhusu mabadiliko ambayo hutokea pale ambapo fonimu mbili huambatana katika kuunda vipashio vikubwa kuliko fonimu, yaani: silabi, mofu na maana. Kwa upande wa Ngowa, (2015), akichambua Nomino-Mkopo za Kigiriyama kutoka lugha ya Kiingereza, anaeleza kuwa irabu za lugha ya Kiingereza zinapitia mageuzi katika michakato mbalimbali ya kimofonolojia ili kuweza kutamkwa vyema katika lugha ya Kigiriyama. Michakato ya kimofonolojia ambayo

inabainika ni uchopekaji wa irabu, udondoshaji wa irabu, ubadala wa irabu, ufupishaji wa irabu na uimarikaji wa irabu.

Mabadiliko haya hutokea kwa sababu ya sauti moja kuathiri nyingine au sauti mbili kuathiriana katika mazingira maalum ya utokeaji. Mifanyiko ifuatayo hujitokeza katika lugha ya Kiswahili, kama ilivyochambuliwa na Ngowa (Keshatajwa):

Udondoshaji wa fonimu; udondoshaji wa fonimu ni hali ya kuondoa kipashio fulani cha kiisimu katika silabi au neno. Katika lugha ya Kiswahili, irabu ndizo hudondoshwa katika nomino, vivumishi, vitenzi na viwakilishi. Mfano,

Wa + ananchi ----- Wananchi----- /a/

Cha + angu ----- Changu ----- /a/

Zi + etu ----- Zetu ----- /i/

Wa + enyewe ----- wenyewe ----- /a/

Maneno haya yanaumbo la nje ambalo husikika na kuandikwa; umbo la ndani ambalo ni jinsi neno limeundwa na mofu zake mbalimbali kabla ya mfanyiko wa kifonolojia na ugeuzi.

Mvutano wa irabu, huu ni mvutano wa irabu unaotokea pale ambapo irabu mbili zinapokabiliana katika maneno, hususan irabu ya juu na ya chini. Irabu ya juu huivuta irabu ya chini na kuzalisha irabu ya kati na kati. Mfano:

Ma + ino -----> meno

Wa + ingi -----> wengi

Wa + itu -----> wetu

Ukakaishaji; ukakaishaji ni badiliko ambalo hutokea pale ambapo fonimu ambazo si za kaakaa gumu zinapokabiliana tunapata fonimu za kaakaa gumu. Mara nyingi sauti /k/ ambayo ni kipasua cha kaakaa laini hubadili na kuwa /tʃ/ kizuiwa cha kaakaa gumu inapokabiliana na baadhi ya irabu. Mfano:

-angu ----- ki + angu ----- changu

Enye ----- ki + enye ----- chenye

A + li + ki + o + nip + a ----- alichonipa

Usilimisho, usilimisho ni athari ya kitamkwa kimoja juu ya kitamkwa kingine kwa kiasi cha kukifanya kile kinachoathiriwa kifanane kimatamshi na kile ambacho kinakiathiri. Athari hiyo huweza kuwa kwa kiasi fulani au huweza kuwa kamilifu. Katika lugha ya Kiswahili usimilisho hutokea pale ambapo fonimu nazali huambatana na fonimu ambayo si nazali na kuunda sauti ambazo tumeiziita vichangamani. Mfano fonimu /m/ ambayo ni nazali inapoambatana na kipasuo /b/ katika neno /mbali/ tunapata changamano /mb/, maneno mengine ni **nje**, **nge**, **ndama**, **ngali**, **nyuma**.

Tangamano la irabu, tangamano la irabu ni mfanyiko ambao hudhihirisha utaratibu wa baadhi ya irabu kuandamana katika mazingira maalum. Hali hii hutokana na ukweli kwamba irabu zinapokaribiana katika mazingira huweza kuathiriana yaani irabu hudondoshwa au huchopekwa, irabu tofauti kuchukua nafasi ya irabu mbili au irabu kukubaliana kuandamana katika mazingira maalum. Mara nyingi mazingira haya huwa katika mnyambuliko wa vitenzi. Mfano, iwapo mzizi wa kitenzi una irabu /e/ na /o/ basi mnyambuliko utakuwa na irabu /e/. Na, iwapo mzizi wa kitenzi una irabu /a/, /i/ na /u/ basi mnyambuliko utakuwa na irabu /i/ kama vile:

Som -----→ som + esh + a -----→ somesha

Chek -----→ chek + esh + a -----→ chekesha

Pig -----→ pig + ish + a -----→ pigisha

Andam -----→ andam + ish + a -----→ andamisha

Kuimarika na Kudhofika kwa Fonimu

Kuimarika kwa fonimu, badiliko hili huhusu fonimu ambazo hutamkwa kwa kutumia nguvu kidogo zinapobadilika zinakuwa fonimu ambazo hutamkwa kwa kutumia nguvu nyingi. Kiswahili kinaumimarishaji wa aina mbili; kitambaza na uyeyushaji.

Mfano, katika kitambaza; ulimi -----→ Ndimi

Mfano, katika kiyayushaji; Mu + ana -----→ mwana /u/→/w/

mi+aka-----→myaka /i/→/j/

Kudhoofika kwa fonimu ni badiliko ambalo hutokea pale fonimu inayotamkwa kwa kutumia nguvu nyingi inapobadilika na kuwa fonimu inayotamkwa kwa kutumia nguvu kidogo kuliko ile ya awali. Katika Kiswahili, badiliko hili hutokea zaidi katika nomino zinazoundwa kutohana na vitenzi. Mfano,

Mpenda → mpenzi /d/ → /z/

Mjengi → mjenzi /g/ → /z/

Ki + akula → chakula /k/ → /tʃ/

Uyeyushaji, uyeyushaji ni badiliko ambalo husababisha baadhi ya irabu kugeuka na kuwa viyeyushi /j/ au /w/ zinapokubaliana katika mazingira maalumu. Mfano;

Mu + ana → mwana

Vi + ake → vyake

Mi + anga → myanga

Mi + iko → mwiko

Athumani, (2015) anachambua zaidi uyeyushaji kwa kulinganisha lugha ya Kiswahili na Kiyao na kusema kuwa uyeyushaji ni mchakato katika mazingira fulani ya kifonolojia ambayo yanaifanya sauti ambayo haikuwa ya kiyeyusho kuwa kiyeyusho. Katika data alizochambua, kuna maneno kadhaa yameonekana kuwa awali kabla ya kutoholewa katika lugha ya Kiswahili hayakuwa na kiyeyusho lakini yalipotoholewa katika lugha ya Kiyao ikatokea kiyeyusho. Baadhi ya maneno hayo ni;

Kiswahili	Kiyao
------------------	--------------

<i>lako.....</i>	<i>lyako</i>
------------------	--------------

<i>langu.....</i>	<i>lyaangu</i>
-------------------	----------------

Kwa jumla maelezo yote hayo yamechambuliwa kwa urefu kutokana na kuwa ndio muongozo wa utafiti huu kwa kuchambua kulingana na kutofautiana kifonolojia kati ya lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi. Maelezo haya yamekuwa ni faafu kwa kuwa utafiti huu ulichukua kanuni hizi kwa kuchambua matamshi ya lahaja hizi mbili. Kipacha, (2003), akichambua lahaja za Kiswahili anaeleza kuwa orodha ya Fonimu za lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi hazina tofauti na zile za lahaja ya Kiunguja (Kiswahili Sanifu). Katika kuchambua sifa za kifonolojia za lahaja hizi anaeleza kuwa lahaja ya Kitumbatu inasifa ya ufifishaji wa /p/ kama ilivyo katika lahaja ya Kimakunduchi, wakati lahaja ya Kitumbatu inasifa ya udondoshaji wa nazali awali ya vikwamizo na vizuio, mfano kazu → kanzu, uka → ondoka, n.k., kutokudondosha /l/ mfano valya → vaa na hata kutofautisha katika upatanisho wa irabu tamati, mfano sono → sioni, sipata → sipati na, nimbi → nimeimba, wakati sifa

hizi hazipo katika lahaja ya Kimakunduchi. Dondoo hii imetoa mifano ya wazi ambayo ilisaidia utafiti huu kuingia ndani zaidi ili kuona kulingana na kutofautiana kifonolojia kati ya lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi.

Athumani, (hapo juu) anaeleza kuwa maneno ya Kiswahili ambayo katika mpaka wa silabi kuna kuwa na irabu mbili ambazo zinapakana, neno hilo linapokopwa linasababisha kuchopekwa kwa kitambaza /l/ ambacho kinaungana na irabu iliyokuwa na hadhi ya silabi kusaidiana kuunda silabi hiyo ili kusawiri muundo wa kawaida wa silabi katika lugha ya Kiyao. Miongoni mwa maneno hayo ni;

Kiswahili Kiyao

Leo.....lelo

Tetea.....tetela

Pua.....lupula

Kiatu.....chilatu

Uchambuzi huu unafanana kabisa na tabia ya lahaja ya Kitumbatu, ambacho kinatabia ya kutodondosha /l/ katika maneno ambayo kwa kawaida yamedondoshwa /l/ katika Kiswahili sanifu. Mfano, leo (Kiswahili sanifu) ----- lelyo (Kitumbatu). Kutokana na hali hii dondo hii ilisaidia utafiti huu kuibua kulingana na kutofautiana kifonoloji katia ya lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi.

2.4 Lahaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu

Wapo wanazuoni wengi waliofafiti lahaja za Zanzibar kama Kipacha, (2003), Polome, (1967) na wengine, ikiwemo lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kipemba. BAKIZA

(2012), wanaeleza kuwa, lahaja ya Kitumbatu inazungumzwa katika eneo lote la kisiwa cha Tumbatu na maeneo ya Kaskazini mashariki na Magharibi nje ya kisiwa hicho kama vile Nungwi, Potoa, Mkwajuni, Matemwe, Pwani Mchangani, Chaani, Donge na Bumbwini. Hata hivyo wazungumzaji wakubwa wa lahaja hii ni Watumbatu wenyewe wa kisiwani, ambapo asilimia kubwa ya msamiati, sauti na matamshi hunasibishwa na wakazi wa huko.

Polome (1967) ameeleza kwamba Kitumbatu ni lahaja ya Kiswahili inayozungumzwa katika kisiwa cha Tumbatu ambacho kipo kaskazini mwa Kisiwa cha Unguja. Mtafiti huyu amekiweka Kitumbatu miongoni mwa lahaja za visiwani, wakati Nurse na Spear (1985) wamekiweka Kitumbatu katika kundi la lahaja za kusini. Madai ya Kipacha (2003) na Maganga (1995) ni kwamba Kitumbatu ni lahaja itumikayo ndani ya kisiwa cha Tumbatu pekee na kwamba sehemu ya Nungwi nje ya kisiwa cha Tumbatu na ncha ya mwisho ya kaskazini mwa kisiwa cha Unguja hutumika vijilahaja vingine.

Ali (2016) akizungumzia Kitumbatu, anasema; Lahaja hii inazungumzwa katika Kisiwa cha Tumbatu. Kisiwa hiki kipo Kaskazini Magharibi ya Kisiwa cha Unguja karibu na ghuba ya Mkokotoni. Kisiwa cha Tumbatu ni sehemu ya Wilaya ya Kaskazini “A” Zanzibar. Wenyiji wa kisiwa hiki wanaitwa Watumbatu. Samsom (1999), anaelezea juu ya matumizi ya lahaja ya Kitumbatu anasema, ushairi wa Mzee Haji Gora ambao ameitunga katika mwaka 1997, Ndani yake mna msamiati uliotumika ambao ni lugha ya Kiswahili cha Tumbatu. Maelezo yote haya yanathibitisha kuwepo kwa lahaja ya Kitumbatu ambayo inazungumzwa katika kisiwa cha Tumbatu na maeneo ya kaskazini mwa kisiwa cha Unguja.

Kwa upande wa lahaja ya Kimakunduchi, hii ni lahaja inayojulikana kwa majina mbalimbali kama vile Kikae, Kihadimu na Kimakunduchi. BAKIZA (2012), wanaeleza kuwa lahaja ya Kimakunduchi huzungumzwa kwa kiasi kikubwa katika maeneo ya Kusini ya Unguja, Zanzibar. Wakimnukuu Chum, (1994) wanaeleza kuwa sehemu kubwa ya Kusini Unguja hutumia Kikae. BAKIZA (hapo juu) wakifafanua zaidi kwa kusema kuwa katika mkoa wa Kusini, hasa wilaya ya Kusini Unguja, kuna miji kama vile Pete, Jozani, Kitogani, Paje, Jambiani, Muungoni, Muyuni, Kizimkazi, Kibuteni, Mtende na Makunduchi yenye ambayo ndio makao makuu ya lahaja ya Kikae, ndio maeneo yanayotumia lahaja hii ya Kikae.

Wanaongezea kwa kusema kuwa utafiti wa hivi karibuni, umegundua, lahaja ya Kimakunduchi inazungumzwa zaidi katika maeneo ya Makunduchi, Jambiani, na Mtende. Baadhi ya maeneo yaliyotajwa hapo juu yameanza kupoteza hadhi ya kuzungumzwa sana Kimakunduchi kutokana na sababu mbalimbli ikiwemo ya kuwa karibu sana na kuathiriwa na Kiswahili sanifu. Maelezo haya yalisaidia utafiti huu kujua ni maeneo gani yaliyobakia na Kimakunduchi asili katika kupata data zilizowezesha kutafiti kulingana na kutofautiana kifonolojia kwa lahaja hii ya Kimakunduchi na lahaja ya Kitumbatu.

Polome (1976) ameelezea kuwa zipo lahaja 15 za Kiswahili, miongoni mwa lahaja hizo ambazo zinazungumzwa kwa upande wa Tanzania ni Kimtang'ata kinachozungumzwa katika mwambao wa Mrima kati ya Pangani na Tanga (Tanzania bara). Kipemba kinachozungumzwa katika kisiwa cha Pemba, Kitumbatu cha Tumbatu, Kihadimu ambacho pia huitwa Kimakunduchi cha kusini Unguja, Kiunguja kinachozungumzwa sehemu ya kati ya Unguja hasa katika mji wa Unguja. Pia,

ameeleza kuwa kuna tofauti baina ya lahaja moja na nyingine. Alionesa tofauti hizo kwa kusema kuwa msamiati wa aina moja huweza kuwa na sauti tofauti. Kwa mfano lahaja ya Kingare hutumia /k/ katika neno kama vile ‘nkewe’ ambapo Chijomvi hutumia /ch/ katika neno hilo hilo na kuwa ‘ncchewe’. Kazi hii ilimuongoza mtafiti kuweza kufikia lengo la kazi yake la kupata mlingano na utofautiano baina ya lahaja hasa katika kipengele cha kifonolojia kama alivyo chambua katika mifano yake hapo juu. Maeleo haya yalitoa namna ya kuweza kuchambua jinsi fonolojia ya lahaja ya Kimakunduchi inavyolingana na kutofautiana na fonolojia ya lahaja ya Kitumbatu.

Maganga (1995), katika kazi yake amechambua lahaja tatu za Zanzibar, lahaja hizo ni lahaja ya Kitumbatu, Kimakunduchi, na Kipemba na kuzihusisha na Kiswahili sanifu. Lengo kuu la kazi hii ni kuchunguza mofofonolojia ya lahaja ya Kitumbatu, Kimakunduchi na Kipemba huku akizihusisha na Kiswahili sanifu kama ilivyo katika mfano hapo chini;

Kiswahili sanifu	Kipemba	Kimakunduchi	Kitumbatu
Mti	nti	ufiti	mfiti
Sisi	sije	suwe	suje
Mimi	mije	miye	mije
Lile	lile	lilya	lile

Dondoo hii inatupa mifano ya misamiati ya lahaja za Zanzibar na namna inavyotofautiana na Kiswahili sanifu hasa katika kipengele cha kifonolojia. Hivyo mfano huu ulikuwa ni muongozo wa kuangalia kulingana na kutofautiana kifonolojia kati ya lahaja ya Kimakunduchi na lahaja ya Kitumbatu.

Nurse na Hinnebusch (1993:522), kwa upande wao wameeleza kwa kusema kuwa uhusiano wa msamiati ya lahaja za Zanzibar huingiza au hudondosha sauti /i/ na/au /y/ mfano katika lahaja za Unguja vijiji ni wanafafanua kuwa; Msamiati wa lahaja za Kitumbatu na Kimakunduchi ambazo ni lahaja za asili za Kaskazini na Kusini zina sifa zifuatazo.

Huingiza au hudondosha sauti |i| na au |y| mfano

Lawa- / yawa- “ondoka”

laga “ aga “

lola-/ yoya “ tazama.”

Huzuia sauti katika maneno yake

-udi “rudi”

-afiki “rafiki”

Kazi hizi zimechambua kwa kina juu ya lahaja zinazopatikana Zanzibar hasa lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi. Kwa kuangalia uhusiano wake, kufanana kwake na tofauti kati ya lahaja hizi. Utafiti huu uliona kunahaja ya kuzamia zaidi katika kuangalia kulingana na kutofautiana kifonolojia kati ya lahaja ya Kimakunduchi na lahaja ya Kitumbatu hasa katika kipindi hiki ambacho maendeleo ya sayansi na teknolojia yamepunguza sana vikwazo vya mawasiliano baina ya eneo moja na jingine.

2.5 Nadharia Zilizotumika Katika Kukusanya na Kuchambua Data za Utafiti

Katika uchambuzi wa data kulitumika msingi na utaratibu maalumu ambao unaitwa nadharia. Massamba (2004:63) anabainisha kuwa nadharia ni taratibu, kanuni na

misingi ambayo hujengwa katika muundo wa mawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kielelezo cha kuelezea jambo. Kwa maana hiyo, fonolojia kama taaluma zingine, nayo huhitaji nadharia katika kushughulikia vipengele vyake. Baadhi ya nadharia zilizokwishaibuliwa mpaka sasa katika taaluma ya fonolojia ni kama vile, fonolojia muundo, fonolojia vipandesauti huru, fonolojia leksika n.k. Kwa hakika nadharia ni msingi au utaratibu unaomsaidia mtafiti katika kukusanya na kuchambua data za utafiti wake. Kama ilivyooneshwa hapo juu, fonolojia ni taaluma yenye nadharia tofauti ambazo huweza kumsaidia mtafiti kupata data na kuchambua data hizo. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia nadharia ya Konsonanti Vokali na nadharia ya Isimulinganishi. Utafiti ultumia nadharia hizi kwa sababu ndizo nadharia zilizosaidia kulinganisha na kutofautisha lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi kwa hoja za kiisimu.

(i) Nadharia ya Konsonanti Vokali

Nadharia ya Fonolojia ya Konsonanti Vokali ni nadharia iliyoasisiwa na Kahn (1976) kuweza kudhibiti uchanganuzi wa silabi za maneno kwa kupambanua mifanyiko mbalimbali ya kifonolojia na kimofolojia inayofanyika katika ngazi ya silabi. Hatimaye nadharia hii ilionekana kuwa na umuhimu mkubwa katika uchanganuzi wa masuala ya kifonolojia na hata ya kimofolojia na hivyo ikapata kuendelezwa na wataalamu kama (Clement na Keyser, 1983; Katamba, 1989; Goldsmith, 1990). Haule (2014) anamnukuu Kahn (1976: 37) anafafanua muundo wa silabi na kusema kuwa;

(i) Kila kipande cha silabi kinahusishwa na silabi moja.

(ii) Kila kipande ambacho hakina hadhi ya silabi kinahusishwa na silabi.

(iii) Mistari inayohusisha silabi na vipande haipaswi kukatizwa.

Kahn (hapo juu) anaingia ndani zaidi kwa kusema kuwa muundo wa silabi unategemea lugha husika na kwamba kama hakuna utambuzi wa silabi ni vigumu kutambua mpangilio wa mofimu katika neno. Katika hali hiyo, nadharia hii ilisaidia kubaini kulingana na kutofautiana kifonolojia kati ya lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi. Uchanganuzi huu, kupitia nadharia hii ya Konsonanti Vokali ulisaidia kujuu sababu za kulingana na kutofautiana kifonolojia katika maneno mbali mbali ya lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi. Nadharia hii ilichanganua silabi katika ngazi tatu ambazo ni ngazi ya silabi (alamu ya silabi), ngazi ya konsonanti vokali na ngazi ya vipande sauti vinavyounda neno (Katamba, 1989; Goldsmith 1990). Kama walivyonukuliwa na Athumani, (2013). Nadharia hii ilisaidia kuchambua lahaja hizi kwa kuangalia namna maneno ya lahaja yanavyolingana na kutofautiana katika muundo wake wa kisilabi na vipande sauti vinavyopatikana katika maneno hayo.

(ii) Isimu linganishi

Utafiti huu ultumia nadharia ya Isimu linganishi. Isimulinganishi ni tawi la Isimu historia linalojishughulisha na ulinganishaji wa lugha ili kuelezea uhusiano wake wa kihistoria. Kiunzi hiki cha kinadharia kinachunguza na kuchanganua lugha tofauti zenyet uhusiano na asili moja. Lehmann akinukuliwa na Mgullu (2001:3) ameeleza kuwa lengo mahususi la Isimulinganishi ni kufanya uchunguzi wa lugha mbalimbali ili kuzilinganisha na pia kuzilinganua.

Kupitia kiunzi hiki, wanaismu huzichunguza lugha katika viwango vyote yaani fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki ili kuonyesha na kuelezea jinsi lugha hizo zinavyofanana au kutofautiana kwa kutumia mbinu linganishi (Campell, 2004), utafiti

huu ulijikita zaidi na kipengele cha kifonolojia. Kanuni ya msingi ya mbinu hii ni kuzilinganisha lugha mbili au zaidi ili kubainisha tofauti na mabadiliko ya mifumo ya fonolojia, kama ambavyo utafiti huu, ulilingalinisha na kutofautisha kati ya lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi.

Mnamo mwaka 1972 nadharia hii ilitumiwa na Raimo Anttila kulinganisha lugha za Kiswidi, Kiingereza na Kijerumani. Anttila, (1972:229) anaeleza: “... *ni mbinu kuu ya Isimulinganishi inayotumiwa kuchambua lugha zaidi ya moja ambazo zina asili moja ili kuanzisha uhusiano wake wa kihistoria*”, (Tafsiri ya Mtafiti).

Katika nadharia ya isimulinganishi kuna vigezo vinavyotumiwa kulinganisha lugha:

- (i) Kigezo cha kwanza ni kuangalia kukubaliana kwa sauti katika maneno. Kulinganisha sauti za msamiati wa lahaja ili kuona ni kwa kiasi gani zinafanana au zinatofautiana.
- (ii) Kigezo cha pili ni kuchunguza ili kuona kama lugha hizo zina maneno yenye mjengeko mmoja kifonolojia na ikiwa zina maana moja au maneno yana maana moja lakini yana sauti tofauti.

Vigezo hivi vilitumika kama ni misingi ya kukusanya na kuchambulia data za utafiti huu ili kupata kulinagana na kutofautiana kifonolojia kwa lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi. Wakati mwingine wanaisimu wanapozilinganisha lugha mbalimbali hufanikiwa kuunda lugha mama, ya lugha hizo, Kutokana na hiyo lugha mama, wanaisimu hubainisha lugha zilizo na uhusiano wa kinasaba na kuonyesha jinsi lugha hizo zinavyotofautiana.

Kwa ujumla, nadharia za isimulinganishi na nadharia ya Konsonenti Vokali zilitumika kusaidia kulinganisha na kutofautisha kifonolojia kati ya lahaja ya Kimakunduchi na lahaja ya Kitumbatu.

2.6 Pengo la Utafiti

Baada ya mtafiti kusoma kazi tangulizi mbalimbali ikiwemo vitabu na tafiti za watafiti waliotangulia aligundua kuwa kwa upande wa asili na chimbuko la lahaja bado kuna utatanishi kwani kila mtafiti anaelezea kulingana na mtazamo wake mwenyewe tu, hakuna mawazo ya jumla yanayothibitisa namna lahaja zilivyoibuka na asili yake. Kwa upande wa tafiti zilizofanywa kuhusu mlingano na tofauti zinazojidhihirisha katika lahaja, kumekuwa na tafiti nyingi zilizochambua suala hilo, ila tafiti hizi zimejikita zaidi katika kulinganisha na kutofautisha lugha za kibantu na lugha ya Kiswahili, mfano kulinganisha Kiya na Kiswahili. Pia, mtafiti amegunduwa kuwa bado kuna haja ya kuchunguza kulingana na kutofautiana kati ya lahaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu kwa kuangalia hasa kulingana na kutofautiana kifonolojia kwa sababu, watafiti wengi waliochunguza tofauti za lahaja hizi, walijikita zaidi katika tofauti za misamiati, matamshi na maumbo yake, kama Bakari (2015) aligusia kipengele hiki kwa lahaja ya Kipemba na Kitumbatu, Maganga (1991) kwa kulinganisha misamiati ya lahaja ya Kitumbatu, Kimakunduchi na Kiswahili sanifu na Kipacha (2003) kwa kuchambua sifa bainifu za lahaja hizi. Hivyo, mtafiti hakuona utafiti ulioangalia uga (uwanja) huu na bado jamii inahitaji kujua taaluma hii ili kujua uhusiano halisi kwa kulinganisha na kutofautisha lahaja hizi.

SURA YA TATU

MBINU NA NJIA ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Mbinu za utafiti zinafafanuliwa na Kothari (2004) kuwa ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa katika kufanya utafiti. Mbinu za utafiti zinaweza kugawanywa katika makundi mawili makubwa, ambayo ni mbinu zitumiwazo kukusanya data na mbinu zitumiwazo katika uchanganuzi wa data. Katika sura hii mtafiti alibainisha taratibu, mbinu na njia mbalimbali zilizotumika katika ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa data za utafiti ili kuchunguza kulingana na kutofautiana kati ya lahaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu. Sehemu hii imemelezea eneo la utafiti, usampulishaji, watoa taarifa na vifaa vya utafiti. Pamoja na vipengele hivyo, vipengele vya ukusanyaji wa data, mbinu za uchambuzi wa data na uwasilishaji wake pia viliezwa katika sehemu hii.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika Zanzibar ambako lahaja ya Kimakunduchi inazungumzwa kusini mwa kisiwa cha Unguja, na lahaja ya Kitumbatu inazungumzwa katika Kisiwa cha Tumbatu na eneo la kaskazini ya Unguja. Kisiwa cha Tumbatu ni kisiwa kidogo sana katika Bahari ya Hindi, chenye urefu wa takriban kilometra 6 na upana wa kilometra 2, ambapo kwenye upande wa mashariki kiko umbali wa takriban kilometra 5 ya bandari ya mkokotoni iliyoko kaskazini Unguja. Kwa upande wa kaskazini na Magharibi kisiwa cha Tumbatu kimepakana na bahari ya hindi. Kisiwa cha Tumbatu kina shehia nne, shehia ya Jongowe, Gomani, Uvivini na shehia ya Mtakuja. Maeneo mengine yanayozungumzwa lahaja hii ni pamoja na Nugwi, Kidoti, Mkwajuni,

Mkokotoni na kadhalika. Mtafiti alifanya utafiti huu katika eneo la ndani ya kisiwa cha Tumbatu. Eneo hilo limechaguliwa kwa kuzingatia kigezo kwamba sehemu hii ya kisiwa cha Tumbatu ndipo inapozungumzwa lahaja ya asili ya Kitumbatu kwa kupata misamiati ya asili na matamshi ya asili ya misamiati hiyo. Pia kila mkazi wa eneo hili hujifaharisha kwa kuzungumza lugha ya uzawa na kujitahidi kwa kiasi kikubwa kujiepusha na athari za Kiswahili Sanifu na lugha za kigeni kutokana na kutengwa na mazingira na hata kutokuwa na mchanganyiko wa wageni wa nje ya Kisiwa hicho. Kutokana na hali hii, lahaja hii imeweza kuwa na mlingano halisi na lahaja ya Kimakunduchi.

Kwa upande mwingine utafiti huu, ulielekea mkoa wa kusini Unguja ili kuangalia lahaja ya Kimakunduchi. Kwa mujibu wa Kipacha, (2003) Kimakunduchi ni lahaja inayojulikana kwa majina mbalimbali kama vile Kikale, Kihadimu au Kikae ingawaje wenyiji hupenda kujiita Wahadimu. Kimakunduchi huzungumzwa sehemu za kusini na mashariki ya Kisiwa cha Unguja. Makunduchu kietimolojia ni sehemu ya udongo mwekundu. Ipo kusini mwa kisiwa cha Zanzibar umbali upatao maili 40 kutoka mjini Unguja.

Lahaja ya Kimakunduchi huzungumzwa pia katika sehemu za Bwejuu na katika baadhi ya vijiji vya Jambiani kwa upande wa pwani ya Kaskazini ya Makunduchi, upande wa Magharibi huzungumzwa sehemu za Kizimkazi, Muyuni na katika kisiwa cha Uzi, sehemu nyingine ambazo hutumia Kimakunduchi ni Mtende, Paje, Muyuni, na kadhalika. Utafiti huu ulijikita zaidi na eneo la Makunduchi, eneo ambalo lina Shehia ya Mzuri, shehia ya Nganani, sheheia ya Kajengwa, Shehia ya Kiongoni na Shehia ya Tasani. Maeneo haya yalichaguliwa kutokana na kuendelea kutumia lahaja

ya asili ya Kimakunduchi ambayo inaukaribu zaidi na lahaja ya Kitumbatu kifonolojia.

3.3 Walengwa wa Utafiti

Walengwa wa utafiti huu waligawanywa katika makundi mawili; jamii ya watafitiwa¹ na sampuli ya watafitiwa.

3.4 Jamii ya Watafitiwa

Makundi ya jamii ya watafitiwa yaliyoshughulikiwa ni haya yafuatayo:

Lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi, hapa utafiti unalenga kupata maneno ya lahaja hizi kwa lengo ya kuyachambua sauti zake au namna ya kutamka; Wataalamu na wahadiri wa lahaja za Kiswahili waliowahi kuzisoma na kutafiti lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya kimakunduchi, lengo ni kusaidia utafiti huu kuchambua kulingana na kutofautiana kwa fonolojia ya lahaja hizi, na;

Wazee wenge umri wa kuanzia miaka sitini (60) na kuendelea wa jamii ya Tumbatu na jamii ya Makunduchi. Hapa mtafiti alilenga kupata taarifa kuhusu namna maneno ya lahaja hizi yanavyotamkwa.

3.5 Sampuli na Usampulishaji

Katika kufikia lengo la utafiti huu, mtafiti atateuwa sampuli maalumu na kwa kwa utaratibu maalumu wa kuipata sampuli hiyo; ambao unaitwa usampulishaji. Kothari, (2004) anaeleza kuwa Usampulishaji ni uchaguzi wa baadhi ya sehemu ya jamii ya

¹ Mambo yote ambayo mtafiti anaweza kuyatumia kwa ajili kupata data za utafiti ikiwemo eneo la utafiti, wahojiwa na maandiko mbalimbali.

utafiti ambayo itaotoa tathimini au taarifa ya jamii nzima. Pia, anaeleza kuwa Usampulishaji ni mchakato wa kupata taarifa kuhusu jamii ya utafiti kwa kuwahoji au kuwatafiti baadhi ya sehemu ya jamii hiyo. Kwa jumla ni hali ya kutafuta baadhi ya wanajamii kwa lengo la kupata taarifa za utafiti husika. Utafiti huu ulitumia sampuli lengwa ili kuweza kupata data zilizohitajika katika kazi hii. Sampuli ni watafitiwa ambao wamechaguliwa kutoka katika kundi au vitu ambavyo vinatafitiwa kutoka katika kundi fulani. TUKI (2004) na Kothari (2009) wanassema sampuli inaweza ikawa ni kitu kimoja kati ya vingi vya aina ileile kinachochukuliwa kama mfano mzuri wa vitu hivyo. Kothari (1993), ameellezea umuhimu wa kutumia usampulishaji kwamba hupunguza utumiaji wa muda mwingi, nguvu na pesa. Katika utafiti huu, ilikuwa vigumu kuhoji watu wote wanaozungumza lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi. Hivyo ni baadhi au sampuli ya watu hao ndio walio hojiwa ili kupata data za utafiti. Mtafiti alitumia sampuli lengwa katika kuwapata watafitiwa.

3.5.1 Sampuli Lengwa

Katika mbinu hii mtafiti hulenga kundi fulani la watu, vitu au dhana zinazoaminika kuwa na uhakika juu ya utafiti husika (Kombo na Tromp 2006). Utafiti huu uliangalia lahaja mbili, lahaja ya Kitumbatu inayozungumzwa katika Kisiwa cha Tumbatu na Kaskazini mwa kisiwa cha Unguja na Kimakunduchi kinachozungumzwa Makunduchi na kusini na Mashariki mwa kisiwa cha Unguja. Utafiti ulifuata mambo yafuatayo katika kupata data zake:

Utafiti huu, ulichambua fonolojia inayopatikana katika maneno yanayopatikana katika lahaja ya Kitumbatu na ya Kimakunduchi, ambapo jumla ya maneno hamsini (50) yamechambuliwa. Majina haya yalipatikana kuitia kwa sampuli ambao walihojia

kwa njia ya usaili na hojaji. Mtafiti alichambua maneno haya na baadae kulinganisha kwa kutumia nadharia ya Isimulinganishi.

Utafati ulihoji sampuli ya watu thelathini (30) inayotoka kisiwa cha Tumbatu na sampuli ya thelathini (30) inayotoka eneo la Makunduchi. Ili kupata mlingano na utofauti wa kifonoloji kwa lahaja mbili hizo.

Utafiti ulizingatia wazee wenye umri wa kuanzia miaka sitini (60) na kuendelea na wataalamu wa lahaja za Kiswahili, sampuli ya wataalamu ilipatikana kwa kuwachagua walimu wanaofundisha somo la Kiswahili na ambao wana kiwango cha angalau stashahada ya Kiswahili. Sampuli ya wazee kwa kawaida inakuwa ndio yenyenye kujenga na kutumia asili ya eneo husika na haiathiriki na mambo ya kisasa au mambo ya kimambo leo. Kwa kutumia mbinu hii, utafiti uliwahoji watu 30 wanaozungumza lahaja ya Kitumbatu kutoka Tumbatu, wazee 20, na wataalamu wa lahaja 10. Uteuwaji wa watu 30 wanaozungumza lahaja ya Kimakunduchi kutoka Makunduchi, wazee 20, na wataalam wa lahaja 10. Hivyo utafiti ulikuwa na jumla ya sampuli ya watu 60, wazee 40 na wataalamu wa lahaja 20. Sampuli ya wazee ilipatikana kwa Mtafiti kuongozwa na wanyeji wa maeneo haya, kwa kuangalia wazee wenye uelewa wa masuala ya lahaja yao na ambao wanaumri wa kuanzia miaka sitini (60) na kuendelea. Na kwa upande wa wataalamu, Mtafiti alitafuta wenyеji wa Lahaja ya Kimakunduchi na Lahaja ya Kitumbatu ambao pia wamesoma lugha ya Kiswahili angalau kwa kiwango cha Stashahada, sampuli hii ilipatikana kwa kuitia walimu wa somo la Kiswahili katika Shule za Tumbatu na Shule za Makunduchi wenye kiwango cha kuanzia stashahada ya Kiswahili. Kwa jumla sampuli ilipatikana kwa njia ya sampuli

lengwa, vigezo maalumu vilivyotumika kama vile; umri kuanzia miaka siti na uwenyeji wa lahaja husika kwa kwa wazee na Stashahada ya Kiswahili likiwemo somo la lahaja au mwenyeji wa lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi kwa sampuli ya wataalamu. Jedwali lifuatalo linaonesha mgawanyo wa Sampuli iliyotumika katika utafiti huu.

Jedwali Na. 3.1: Mgawanyo wa Sampuli Iliyotumika katika Utafiti Huu

Lahaja ya Kitumbatu		Lahaja ya Kimakunduchi	
Lahaja ya Kitumbatu	Idadi	Lahaja ya Kimakunduchi	Idadi
Wazee	20	Wazee	20
Wataalamu wa Lahaja	10	Wataalamu wa Lahaja	10
Jumla	30	Jumla	30

Chanzo cha data hii ni mtafiti,(2018)

Mtafiti alitumia mbinu hii ya sampuli lengwa kwa lengo la kukidhi na kufikia vigezo vya sampuli iliyoelezwa hapo juu.

3.6 Mbinu za Kukusanya Data

Utafiti huu ulitumia mbinu za aina mbili. Mtafiti alifikia uamuzi wa kutumia mbinu za aina hiyo ili kupata uthabiti wa matokeo ya utafiti aliokusudia kuufanya. Mbinu zilizotumika katika utafiti huu ni:

- (i) Hojaji
- (ii) Mahojiano

3.6.1 Hojaji

Hojaji ni miongoni mwa mbinu zinazotumika kukusanya data. Kwa mujibu wa Kothari (2004) hojaji ni mbinu ya kukusanya data ambapo mtafiti huandika maswali

na kisha kuyapeleka kwa watoa taarifa ili wayajibu na baadae kumrudishia mtafiti yakiwa tayari yemeshajibiwa. Walliman (2011), anaongeza kuwa maswali ya hojaji yako ya aina mbili; aina ya kwanza ni ile inayohusisha maswali fungo ambayo hutoa fursa kwa watafitiwa kuchagua jibu mionganoni mwa majibu kadhaa yaliyopendekezwa.

Aina hii ya hojaji ni rahisi kujibu na inasaidia kupata majibu mahsusini na huepusha upendeleo. Aina ya pili ya maswali ya hojaji ni ile inayohusisha maswali yasiyo fungo ambayo hutoa fursa kwa watafitiwa kuwa huru kueleza wanachokijua juu ya dhana fulani kutegemeana na kile kilichoulizwa. Aina hii hutoa uhuru kwa watafitiwa kueleza mawazo yao kwa ubainifu na uwazi na pia husaidia kupata taarifa nyingi zaidi.

Mbinu hii ya hojaji ilitumika katika utafiti huu na ilijumuisha aina zote mbili za maswali yaliyokuwemo katika hojaji; yaani maswali fungo ambayo yalikuwa ni matatu na maswali yasiyofunge ambayo yalikuwa ni maswali saba. Kwa sababu kila moja kati ya aina hizi mbili za hojaji zilimsaidia mtafiti kupata data za kina juu ya kulinagana na kutofautina kwa lahaja hizi pamoja na sababu za kulingana na kutofautiana huko. Maswali haya, ya hojaji yaligusa katika malengo yote matatu ya utafiti huu.

Hojaji lilitumika kwa Sampuli ya Wataalamu wa lahaja tu (hawa ni wale wenyeji wa Tumbatu na Makunduchi na wanataaluma ya lugha ya Kiswahili angalau Stashahada) ambao idadi yao walikuwa (20), kutoka katika lahaja ya kimakunduchi (10) na lahaja ya kitumbatu (10), ili kuwapa fursa watafitiwa hao kutoa maelezo yakina na yenye hoja za kitaaluma.

3.6.2 Mahojiano/Usaili

Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006), mahojiano ni majibizano ya ana kwa ana au ya simu, barua pepe na kadhalika yanayofanyika kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti lililoainishwa. Walliman (keshatajwa) ameyagawa mahojiano katika aina tatu ambazo ni mahojiano ya ana kwa ana, mahojiano ya kikundi na mahojiano ya simu (mtandao).

Kwa mujibu wa Kothari (2009), mahojiano ya ana kwa ana ni mbinu ambayo mtafiti huwaauliza maswali watafitiwa na wakati mwingine watafitiwa hupata fursa ya kumuuliza maswali mtafiti. Ingawa mbinu hii inaweza kufanywa kwa njia zote hizo, mtafiti alitumia mbinu ya ana kwa ana kuwahoji watafitiwa wake, ili kupata data za lahaja ya Kimakunduchi na lahaja ya Kitumbatu ana kwa ana. Katika mbinu hii walihojiwa wazee 20 kutoka kila lahaja na kufanya jumla ya wazee 40 kwa lahaja mbili. Wazee ambao walipatikana kutokana na muongozo wa masheha wa maeneo husika kwa kuwachaguwa wazee waliofikia umri wa miaka sitini na kuendelea na wenyе umahiri katika masuala ya lahaja zao.

Mtafiti alitumia mbinu hii kwa sababu kadhaa; kwanza, ni kwa ajili ya kupata uthabiti wa majibu ya watafitiwa. Pili, ni rahisi kwa mtafiti kudhibiti sampuli yake kwa wepesi na kwa usahihi zaidi. Hii inawezekana kwa sababu mtafiti alikuwa na fursa ya kuwahoji ana kwa ana na kuwaauliza maswali na kurekodi majibu yao papo kwa papo wakati mahojiano yao yanaendelea, kama ni sehemu ya ushuhudiaji wa matamshi. Mbinu ya kurikodi ilimsaidia mtafiti kurikodi sauti ambazo zilikuwa ni ngumu kuziandika kwa ghafla kama vile sauti “ly” na “lw” ambazo zilimbidi mtafiti kutafuta msada kwa wataalamu wenyеji wa lahaja ya Kitumbatu ili kupata tahajia zake. Pia

maswali ambayo yalikosa majibu yaliweza kutafutiwa ufumbuzi papo kwa papo. Tatu, ilikuwa ni rahisi kwa mtafiti kukusanya taarifa nyingi na kwa kina zaidi. Kwa sababu watafitiwa waliweza kuulizwa maswali na mtafiti alikuwa na uhuru wa kuuliza maswali ya ziada. Fursa hii ilikuwa haipatikani katika mbinu nyingine za kukusanya data, kama vile hojaji na nyinginezo. Mbinu ya mahojiano ilitumika kukusanya data katika sampuli ya wazee, hii ni kutokana na wazee wengi walikuwa hawajui kusoma na kuandika au kuwa wazito wa kuandika kwa wale wanaojua. Pia mbinu hii ilichunguza matamshi halisi ya msamiati unavyotumika kwa kila upande wa lahaja. Mbinu hii mtafiti alifaidika zaidi kwa kupata data zinazohusiana na sababu za lahaja hizi kufanana na kutofautiana kutokana na historia walizokuwa wakitowa wazee wa Tumbatu na Makunduchi.

3.7 Vifaa na Zana za Kukusanya Data

Utafiti ulifanyika kwa ufanisi kwa sababu ulijumuisha vifaa na zana mbalimbli katika mchakato wa maandalizi ya utafiti, ukusanyaji wa data, uchambuzi wa data na hata hatua ya kuandika tasnifu ya utafiti. Utafiti huu ilitumia vifaa na zana zifuatazo katika kukusanya na kuchambua data pamoja na kuandika tasnifu:

Kamera za picha mgando, zana hii ilitumika zaidi katika hatua ya kukusanya data. Mtafiti alitumia kamera kwa lengo la kuweka kumbukumbu za utafiti, kama vile kuweka picha za wahojiwa na hata maeneo muhimu, yaliweza kusaidia ufanisi wa utafiti huu.

Kinasa sauti, zana hii nayo ilitumika katika hatua ya kukusanya data za utafiti huu, lengo la zana hii ni kumsaidia mtafiti kuhifadhi data, hasa kwa ile njia ya mahojiano, njia ambayo inakuwa ngumu kuhifadhi data zake kwa mara moja au kuziandika kwa

mara moja tena kwa ufanisi. Hivyo ili kurahisisha hatua hii, mtafiti alitumia kinasa sauti kunasa data za mahojiano.

Komputa, zana hii ilitumika kwa kila hatua kama vile maandalizi kwa kuandika pendekazo la utafiti, ukusanyaji wa data kwa kutunzia kumbukumbu ya data zilizokusanywa na uchambuzi wa data katika kurahisisha mchakato wa kuchambua data na mwisho kuandikia tasnifu ya utafiti huu.

3.8 Mkabala wa Kuchambua na Kufafanua Data

Data katika utafiti zilichambuliwa na kufafanuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo (kiufafanuzi). Enon (1998) akichambua mkabala wa kimaelezo, anaeleza kuwa mkabala usio wa kiidadi ni mbinu ya kuchambua na kufafanua data ambapo mtafiti hueleza na kubainisha data zake kwa kutumia maelezo. Aidha, Kress (2008) anafafanua mkabala huu kuwa unaelezea vipi na kwa nini matukio yametokea. Kutokana na maumbile ya kazi yake, katika utafiti huu mtafiti alijikita zaidi kwenye uchambuzi unaozingatia mkabala usio wa kiidadi. Mbinu hii ilitumika kwa sababu, mtafiti alijishughulisha na maswali ya lugha. Lugha inahitaji usahihi wa vipashio vitumikavyo kujenga lugha hiyo, bila kuzingatia sana wingi au uchache wa idadi ya wazungumzaji.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Katika sura hii, data zilizokusanywa zimewasilishwa na kujadiliwa ili kujibu maswali ya utafiti, na hivyo kufikia malengo ya utafiti. Uwasilishaji wa data umegawanywa katika sehemu zifuatazo: kwanza, orodha ya msamiati uliokusanywa katika kazi hii. Pili, ulinganishi wa matamshi kati ya lahaja ya Kimakunduchi na lahaja ya Kitumbatu. Tatu, tofauti za matamshi kati ya lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi. Nne, sababu za kufanana na kutofautiana kati ya lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi. Na mwisho, ni hitimisho la sura hii.

4.2 Uwasilishaji wa Msamiati wa Lahaja ya Kitumbatu na Lahaja ya Kimakunduchi

Kazi hii imekusanya na kuchambua jumla ya maneno hamsini (50), kutoka lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi kwa lengo la kuchambua fonimu zake zinazozilingana na kutofautiana. Misamiati hii imechukuliwa ile tu yenyе maumbo ya aina moja, kuwa na maana moja na kuwa na matumizi yenyе kulingana katika lahaja hizi. Katika uchambuzi msamiati huu umegawiwa katika makundi mawili. Msamiati wenyе fonimu zenyе kulingana katika lahaja hizi mbili, na msamiati wenyе mofimu zenyе kutofautina. Jedwali la Misamiati ya Lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi.

**Jedwali Na. 4.1: Msamiati wa Lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi
Uliokusanywa kwa Lengo la Kuchambuliwa Kufanana na
Kutofautiana kwake**

Na.	Msamiati wa Lahaja ya Kitumbatu (Kt)	Msamiati wa Lahaja ya Kimakunduchi (Km)	Msamiati wa Kiswahili Sanifu (Ks)
1.	Azini	Azini	Adhini
2.	Kanasoma	Kasoma	A nasoma
3.	Dawia	Daukia	Amkia
4.	Usende	Usende	usiende
5.	Koga	Koga	Oga
6.	Chavumbika	Savumbika	Nitavumbika
7.	Pya	Pya	Mpya
8.	Singo	Singo	Shingo
9.	Lamba	Lyamba	Ramba
10	Jibwe	Jibwe	jiwe
11.	Dicho	Dicho	Jicho
12.	Randa	Randa	Zurura
13.	Nyende	Nyende	Niende
14.	Kwenda	Kwenda	Kuenda
15.	Yenga	Jenga	Jenga
16.	Futuru	Futuru	futari
17.	Fyagio	Fyagio	Fagio
18.	Kyende	Kende	Kaenda
19.	Kugwisha	kugwisha	kuangusha
20.	Kwima	Kwima	Simama
21.	Chuza	Angalia	Angalia
22.	nyevu	nivu	nilikuwa
23.	kibali	kibali	kibali
24.	Nkwambii	Nikwambili	Nimekwambia
25.	mvisi	mpishi	mpishi
26.	vano	pano	- (hapa)

27.	Yalibu	Jaribu	Jaribu
28.	Nyevu	Nivu	Nilikuwa
29.	kukwea	kukwelya	kukwea
30.	Vasuka	Pasuka	Pasuka
31.	chasoma	Sasoma/tasoma	Ntasoma
32.	kevu	kavu	Alikuwa
33.	Biringita	Biringia	Zunguka
34.	nyuwe	nyuye	nyiye
35.	fwana	Fana	Fana
36.	Suwe	Suye	Siye
37.	Silitenda	sijatenda	sijatenda
38.	Ipu	Jipu	Jipu
39.	Luka	Ruka	Ruka
40.	vua	Vulya	mvua
41.	kengewa	kengeza	kengeza
42.	Bofu	Tafya	Bofu
43.	kifwefwe	Kifyefye	kifyefye
44.	kigugumsi	kigugumizi	kigugumizi
45.	Tavika	Sapika	nitapika
46.	kilevu	kidevu	kidevu
47.	howiza	himiza	himiza
48.	kidigi	kidogo	kidogo
49.	Boti ya Mzigo	Vera	Boti ya Mizigo
50.	Zamana	Zamana	Dhamana

Chanzo: utafiti, 2018

Jedwali hili limejumuisha msamiati wote uliokusanywa na mtafiti kwa lengo la kuchambua kufanana na kutofautiana kwa msamiati wa lahaja hizo katika matamshi (fonolojia yake). Msamiati huu ulipatikana baada ya upembuzi na uchambuzi kutokana na data zilizokusanywa katika utafiti huu, kupitia sampuli ya utafiti huu.

4.3 Ulinganifu wa Fonimu za Lahaja ya Kimakunduchi na ya Kitumbatu

Utafiti umebaini kuwa, kuna ulinganifu mkubwa wa kimatamshi kati ya lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi katika fonimu zake. Mionganini mwa fonimu hizo ni:

Jedwali Na. 4.2: Ulinganifu wa Fonimu za Lahaja ya Kitumbatu na Lahaja ya Kimakunduchi

Fonimu za Lahaja ya Kitumbatu (Kt)	Fonimu za Lahaja ya Kimakunduchi (Km)	Fonimu za Kiswahili Sanifu (Ks)
zini - /z/	azini - / z /	adhini - /ð/
kanasoma - /k/	kasoma - /k/	anasoma - /a/
/e/ – usende	/e/ – usende	/ie/ - usiende
/k/ – koga	/k/ – koga	/o/ – oga
Ø – pya	Ø – pya	/m/ – mpya
/s/ – singo	/s/ – singo	/ʃ/ – shingo
/bw/ – jibwe	/bw/ – jibwe	/w/ – jiwe
/d/ – dicho	/d/ – dicho	/j/ – jicho
/nj/ – nyende	/nj/ – nyende	/n/ – niende
/kw/ – kwenda	/kw/ – kwenda	/k/ – kuenda
/u/ – futuru	/u/ – futuru	/a/ – i – futari
/fj/ – fyagio	/Fy/ – fyagio	/f/ – fagio
/gw/ – kugwisha	/gw/ – kugwisha	/ŋ/ – kuangusha
/kw/ – kwima	/kw/ – kwima	/s/ – simama
/v/ – nyevu	/v/ – nivu	/k/ – nilikuwa

Mlingano wa fonimu wa lahaja ya Kitumbatu umechambuliwa zaidi na namna fonimu hizo zinavyotofautiana na lahaja ya Kimakunduchi. Pamoja na kuchambua athiri zake katika mazingira maalum ya utokeaji.

4.3.1 Kuwa na Tabia ya Kudondosha Fonimu

Lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi zimekuwa na tabia za kudondosha fonimu katika baadhi ya silabi zake. Hivyo, fonimu iliyobaki huweza kubeba dhima za fonimu nyingine zilizodondoshwa. Hali hii inatokana na msingi unaoeleza kuwa

kipande cha silabi kinaweza kuhusishwa na silabi kamili katika lugha. Maelezo haya yanakubalina moja kwa moja na utafiti uliofanywa na Kombo, (2015) na kuwanukuu, Lambert na Chum (1962) na Hurskainen (1989) kwa kusema kuwa lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi zinatabia ya kudondosha sauti za nasali katika baadhi ya msamiati wake. Kama vile “ugovi” katika neno ugomvi, “cha” katika neno ncha na mengineyo. Utafiti huu, umeenda mbali zaidi na kubaini kuwa lahaja hizi haziishii tu kudondosha sauti za nazali bali hata sauti ambazo sionazali, kama inavyochambuliwa hapo chini:

(a) /n/ – chi (Km) → /n/ – chi (Kt) -----> nchi (Ks)

Fonimu /n/ katika lahaja mbili hizi imekuwa ikidondoshwa katika meneno ya aina kama hii. Lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi imekuwa ikidondosha fonimu za nasali katika baadhi ya maneno kama vile “nge” badala ya nnge, “mbu” badala ya mmbu na mengine kama haya.

(b) /e/ - usende (Km) → /e/ - usende (Kt) -----> /i/ na /e/ - usiende (Ks)

Fonimu /e/ ambayo inatumika katika lahaja ya Kitumbatu na ya Kimakunduchi na inawakilisha fonimu mbili ikiwa neno hili linatumika katika Kiswahili sanifu. Inawakilisha fonimu ya /i/ na /e/, ambapo fonimu /i/ inatumika kuunda silabi ya “si” ambayo ni mofimu yenyeye dhima ya ukarusha na fonimu /e/ ni silabi inayojitegemea na inadhima ya kuunda mzizi wa neno “end” kwa kushirikiana na fonimu “nd”.

4.3.2 Usilimisho

Usilimisho ni athari ya kitamkwa kimoja juu ya kitamkwa kingine kwa kiasi cha kukifanya kile kinachoathiriwa kifanane kimatamshi na kile ambacho kinachokiatiri.

Athari hiyo huweza kuwa kwa kiasi fulani au huweza kuwa kamilifu. Katika lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi zimekuwa na mfanano wa kusilimisha fonimu kwa baadhi ya maneno. Mfano fonimu /b/ ambayo ni fonimu ya kipasuo ikiambatana na fonimu /w/ ambayo ni nusu irabu hutolewa fonimu changamani. Maelezo haya yanaungwa mkono na Kipacha, (2003) wakati wa kuchambua sifa bainifu za kifonolojia anasema kuwa lahaja ya Kimakunduchi inatabia ya kuwa na fonimu zenye utokeaji wa Konsonanti na viyeyusho sifa ambayo inapatikana katika lahaja ya Kitumbatu. Mfano:

(c) /bw/ - jibwe (Km) → /bw/ - jibwe (Kt) -----→ /w/ - jiwe (Ks)

Lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi zinatumia fonimu /bw/ katika neno “jibwe” na katika Kiswahili sanifu inatumiwa fonimu /w/ katika neno “jiwe”. Pia, lahaja hizi zinatumia fonimu /bw/ kwa kuweka irabu ya /e/ na kufanya neno kamili ambalo ni “bwe” ambalo katika Kiswahili sanifu linabakia kwa maana ya “jiwe”

4.3.3 Kuimarisha na Kudhoofisha Fonimu

Lahaja zinachukua sifa zote mbili, kuimarisha na kudhofisha fonimu. Ni dhana zilizoendana kwa kutegemeana hata hivyo, dhana hizi kila moja huweza kujitegemea wenye kama sifa inayoltinganisha lahaja hizi.

4.3.3.1 Kuimarisha Fonimu

Lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi zimefanana katika kuimarisha fonimu ambazo hutamkwa kwa kutumia nguvu kidogo katika Kiswaili sanifu na kuzibadilisha kwa kuzitamka kwa kutumia nguvu nyingi. Hali hii imejitokeza zaidi kwa fonimu ya /l/ ambayo ni kitambaza, fonimu /w/ ambayo ni nusu irabu na hata fonimu /u/ ambayo ni irabu. Mfano:

- (a) Kitambaza; kula (Ks) -----→ kulya (Kt) na (Km) /l/ → /lj/
- (b) Nusu irabu; uwongo (Ks) -----→ ulwongo (Kt na Km) /w/ → /lw/
- (c) Irabu; ua (Ks) -----→ Ulwa (Kt) /a/ → /lw/
- (d) Irabu; ua (Ks) -----→ Lwua (Kt) /u/ → lw/

Utafiti umebaini kuwa fonimu hizi /ly/ na /lw/, hazijawa na otografia halisi inayofahamika na wasomi hasa wa kiwango cha chini. Pia fonimu hizi zimekuwa ni ngumu kutamka kwa mtu ambaye si mwenyeji wa lahaja hizi mbili. Fonimu /l/ imekuwa na fonimu mbili tofauti katika lahaja mbili hizi. Katika lahaja ya Kitumbatu fonimu /l/ katika neno “kula” inatumia fonimu /ly/ katika “kulya” na fonimu /l/ katika neno “lala” inatumia fonimu /lw/ na kupata neno “lwalwa” katika lahaja ya Kitumbatu. Hali pia, inajitokeza katika fonimu /a/ na fonimu /u/ ambazo hutoa fonimu /a/ na /lw/ kama mfano wa hapo juu na fonimu /u/ na /lw/ kama ilivyo chambuliwa katika mfano wa hapo juu. /ly/ na /lw/ si fonimu rasimi bali ni ulinganishaji wa matamshi na maeneo inapotamkiwa.

4.3.3.2 Kudhoofika kwa fonimu

Kudhofika kwa fonimu ni badiliko ambalo hutokea pale fonimu inayotamkwa kwa kutumia nguvu nyingi inapobadilika na kuwa fonimu inayotamkwa kwa kutumia nguvu kidogo kuliko ile ya awali. Sifa hii inapatikana katika lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi. Kombo, (2015) naeleza kuwa lahaja ya Kimakunduchi imekuwa na tabia ya kudhoofisha sauti zake. Kipacha, (2003) naeleza kuwa lahaja ya Kitumbatu inatabia ya ufifishaji wa /p/ kama ilivyo Kimtangata na Kimakunduchi. Hivyo ni wazi kuwa fonimu ambazo ni nzito katika Kiswahili sanifu huweza kurahisishwa na kutamkwa kwa wepesi katika lahaja hizi. Badiliko hili hutokea kwa

maneno ya mkopo, maneno yanayoongezwa fonimu na maneno yanayokazwa kwa
kuwekewa sauti za nasali. Mfano,

- (a) Maneno ya mkopo;

Azini (Kt na Km) → adhini (Ks)

/z/ → /ð/

Utafiti ulibaini kuwa lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi zimekuwa na sifa ya kudhoofisha fonimu /dh/ kutoka katika maneno ya mkopo hasa ya kiarabu na kuweka fonimu /z/ kama ilivyo katika mfano wa hapo juu. Kpunguza ira.

4.4 Tofauti za Fonimu kati ya Lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi

Utafiti umebaini kuwa, kumekuwa na tofauti za kimatamshi kati ya lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi katika fonimu zake.

Jedwali Na. 4.3: Tofauti za Fonimu za Lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi

Fonimu za Lahaja ya Kimakunduchi (Km)	Fonimu za Lahaja ya Kitumbatu (Kt)	Fonimu za Kiswahili Sanifu (Ks)
/l ^h / – kibali	/l/ – kibali	/l/ – kibali
/s/ – mvisi	//Sh – mpishi	//Sh –mpishi
/v/ – vano	/p/ – pano	- (hapa)
//Ny – /e/ – nyevu	/n/ – /i/ – nivu	/n/ – /i/ – nilikuwa
/a/ – kukwea	/ly/ – kukwelya	/a/ – kukwea
//Ch – chasoma	/s/ – /t/ – sasoma/tasoma	/n/ – ntasoma
/e/ – kevu	/a/ – kavu	/a/ – alikuwa
/w/ – nyuwe	/j/ – nyuye	/j/ – nyiye
Fw – fwana	/f/ – fana	/f/, – fana
/l/ – silitenda	/j/ – sijatenda	/j/ – sijatenda
/i/ – ipu	/j/ – jipu	/j/ – jipu
/a/ – vua	/lj/ - vulya	/a/ – mvua
/w/ – kengewa	/z/ – kengeza	/z/ – kengeza
/fw/ – kifwefwe	/fj/ - kifyefye	/fj/ – kifyefye
/s/ – kigugumsi	/z/ – kigugumizi	/z/ – kigugumizi
/l/ – kilevu	/d/ – kidevu	/d/ – kidevu
/w/ – howiza	/m/ – himiza	/m/ – himiza
/i/ – kidigi	/o/ – kidogo	/o/ – kidogo

Utafiti umebaini kuwa kunatofauti kubwa kati ya lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi. Fonoloji ya lahaja ya Kitumbatu ni tofauti na fonoloji ya Kimakunduchi. Suala hili limethibitishwa kutokana na tofauti ya fonimu za lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi. Uchambuzi huu umetokana na nadharia ya Konsonenti Vokali ambayo inaeleza kuwa kipande cha silabi kinahusishwa na silabi moja. Pamoja na msingi wa nadharia ya Isimu linganishi, unaoelezwa kuwa; lahaja huweza kukubaliana au kutofautiana kwa sauti katika maneno ili kuona ni kwa kiasi gani zinafanana na zinatofautiana. Hivyo kipengele hiki kinatofautiana katika mfumo wa vipande vya silabi kujihusisha na silabi moja iliyokamilika.

4.4.1 Ukakaishaji

Ukakaishaji ni badiliko ambalo hutokea pale ambapo fonimu ambazo si za kaakaa gumu zinapokabiliana tunapata fonimu za kaakaa gumu. Katika msingi wa nadharia ya Isimu linganishi, inaelezwa kuwa; lahaja huweza kukubaliana au kutofautiana kwa sauti katika maneno ili kuona ni kwa kiasi gani zinafanana na zinatofautiana. Hivyo, lahaja ya Kimakunduchi imekuwa na tabia ya kukakaisha fonimu /s/ ambayo ni kitambaza cha meno na kuwa /tʃ/ kizuiwa cha kaakaa gumu. Fonimu hii ambayo ni kipande cha silabi kinahusiana na silabi ya /sa/ na /cha/ ambazo zinaingia katika kiwango cha kimofimu.

Kombo, (2015) anaeleza kuwa “Neno takuja linatamkwa chakuja kwenye matamshi ya Kimakunduchi hivyo fonimu /t/ inabadilika nakuwa /č/. Mofimu \$sa\$ (Kt) na \$cha\$ (Km) zinabeba dhima ya nafsi ya kwanza umoja pamoja na njeo ya wakati ujao.

Mfano:

Sasoma (Kt) -----> Chasoma (Km) /s/ → /tʃ/

Fonimu /s/ ya lahaja ya Kitumbatu inatofautinana na /ʃ/ ya lahaja ya Kimakunduchi. Fonimu hizi zinaunda silabi ya \$ sa \$ na \$ cha \$ na kwa sababu zote ni fonimu zenye dhima sawa zinadhihirisha uhisiano wa lahaja mbili hizi na kuonesha kuwa ni zenye asili moja.

4.4.2 Kuimarika na Kudhoofika kwa Matamshi ya Fonimu

Kuimarika kwa fonimu, hii ni hili ya kutamka fonimu kwa kutumia nguvu nyingi badala ya hai ya kawaida ya fonimu hiyo kutamkwa kwa kutumia nguvu kidogo. Katika msingi wa nadharia ya Isimu linganishi, inaelezwa kuwa; lahaja huweza kukubaliana au kutofautiana kwa sauti katika maneno ili kuona ni kwa kiasi gani zinafanana na zinatofautiana. Hali hii inajenga tofauti katika lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi. Lahaja ya Kimakunduchi inatabia ya kuimarisha fonimu mbali mbali na kuonekana kudhofishwa katika lahaja ya Kitumbatu. Mfano:

- (a) Fonimu /l/ kutamkwa kwa nguvu kubwa, kiasi cha kuifanya kwa ni /l/ nzito. Wakati inatamkwa katika hali ya kawaida katika lahaja ya Kitumbatu. Utafiti wa Bakari, (2015) unaeleza kuwa Kitumbatu hutumia zaidi sauti /l/ badala ya /r/ katika matamshi yao. Mfano:

Kibali (Kt) -----> kibali (Km) /l/ → /l^h/

Skuli (Kt)-----> Sukuli (Km) /l/ → /l^h/

Fonimu /l/ katika lahaja ya Kitumbatu kwa maneno kama haya inakuwa ni /l/ ya kawaida kama ambavyo inatamkwa katika Kiswahili sanifu. Tofauti na lahaja ya Kimakunduchi fonimu /l/ katika maneno kama haya inakuwa ni nzito, na hivyo kuonekana ni fonimu inayotofautiana kimatamshi na lahaja ya Kitumbatu. Pamaja na tofauti hii ya kimatashi bado fonimu hizi zinatengeza silabi ya aina moja na kuunda

neno lenye maana moja katika lahaja zote mbili. Kwa mujibu wa nadharia ya Konsonent Vokali, hali hii imedhihirisha kuwa lahaja hizi zinauhusiano wa karibu na ni ushahidi kuwa ni lahaja zenye asili moja.

Kudhoofika kwa fonimu ni badiliko ambalo hutokea pale fonimu inayotamkwa kwa kutumia nguvu nyingi inapobadilika na kuwa fonimu inayotamkwa kwa kutumia nguvu kidogo kuliko ile ya awali. Katika Kiswahili, badiliko hili hutokea zaidi katika maneno ya lahaja ya Kimakunduchi ambyo ni tofauti na lahaja ya Kitumbatu. Mfano,

Kengewa (Km) → Kengeza (Kt) /w/ → /z/

Kigugumsi (Km) → Kigugumizi (Kt) /s/ → /z/

Mvisi (Km) → Mpishi (Kt) /s/ → /ʃ/

Kilevu (Km) → Kidevu (Kt) /l/ → /d/

Silitenda (Km) → Sijatenda (Kt) /l/ → /j/

Ipu (Km) → Jipu (Kt) Ø → /j/

Howiza (Km) → Himiza (Kt) /w/ → /m/

Katika maneno hayo hapo juu, yanadhihirisha tofauti ya fonimu za lahaja ya Kimakunduchi na lahaja ya Kitumbatu. Lahaja ya Kimakunduchi katika baadhi ya mazingira inadhofisha fonimu /z/ na kuifanya kuwa fonimu /w/ na baadhi ya mazingira inadhofisha fonimu hiyo hiyo /z/ na kuwa /s/. Fonimu /s/ katika lahaja ya Kimakunduchi hudhofishwa kutokana na fonimu /ʃ/ inayotumika katika lahaja ya Kitumbatu pamoja na Kiswahili sanifu. Pia, lahaja ya Kimakunduchi kuna baadhi ya mazingira inadhofisha fonimu /j/ na /d/ kutoka katika lahaja ya Kitumbatu na kutumia fonimu /l/ kwa fonimu zote mbili hizo. Wakati mwingine lahaja ya Kimakunduchi inadondosha kabisa fonimu ili kudhofisha silabi husika kama vile silabi “I” ya neno

“Ipu” (Km) ambayo ni sawa na silabi “Ji”. Silabi hii inatoka katika neno “Jipu” katika lahaja ya Kitumbatu. Maelezo yote haya yamedhihiridhwu katika mifano ya hapo juu.

4.4.3 Uyeyushaji

Uyeyushaji ni badiliko ambalo husababisha baadhi ya irabu kugeuka na kuwa viyeyushi /y/ au /w/ zinapokubaliana katika mazingira maalumu. Katika msingi wa nadharia ya Isimu linganishi, inaelezwa kuwa; lahaja huweza kukubaliana au kutofautiana kwa sauti katika maneno ili kuona ni kwa kiasi gani zinafanana na zinatofautiana. Hali hii hutokea kwa lahaja moja kutumia irabu na nyininge kuyeyesha irabu hiyo katika neno lenye muundo sawa na maana moja na kujenga tofauti katika lahaja hizo. Mfano;

a. Nieu → nyevu (Km) /e/ → /j/

Nieu → nivu (Kt) /e/ → Ø

b. Nyie → nyuwe (Km) /i/ → /j/, /e/ → /w/

Nyie → nyuye (Kt) /i/ → /j/, /e/ → /y/

4.4.4 Tofauti Nyininge

Lahaja ya Kimakunduchi na lahaja ya Kitumbatu zimekuwa na tofauti katika mazingira mbali mbali ya fonimu zake, ukitoa zile zilizochambiliwa hapo juu. Tofauti zote hizo zimezingatia msingi wa nadharia ya Isimu linganishi, unaoelezwu kuwa; lahaja huweza kukubaliana au kutofautiana kwa sauti katika maneno ili kuona ni kwa kiasi gani zinafanana na zinatofautiana. Miongoni mwa tofauti hizo ni:

Lahaja ya Kimakunduchi imekuwa maarufu kwa kutumia fonimu /v/ ambayo inatofautiana na fonimu /p/ inayotumika katika lahaja ya Kitumbatu na Kiswahili

Sanifu. Fonimu /v/ imekuwa ni utambulisho mkubwa unaotofautisha lahaja ya Kimakunduchi na lahaja zote za Zanzibar ikiwemo lahaja ya Kitumbatu. Mfano wa maneno yanayotumia fonimu hii ni:-

Mpishi (Kt) → Mvisi (Km) /p/ → /v/

Pita (Kt) → Vita (Km) /p/ → /v/

Pano (Kt) → Vano (Km) /p/ → /v/

Kuogeza viyeyusho kwa baadhi ya fonimu na kufanya kuwa fonimu ambata. Lahaja ya Kimakunduchi imekuwa na sifa ya kuongeza viyeyusho kwa baadhi ya fonimu au kubadilisha viyeyusho hivyo, sifa hii inaelezwa na Kipacha, (2003) kama ni sifa za kifonolojia kwa kusema kuwa lahaja ya Kimakunduchi inasifa ya kuchanganya Konsonanti na viyeyusho, kama “fw” na “vw” na kufanya tofauti na viyeyusho vinavyotumika katika lahaja ya Kitumbatu. Fonimu maarufu ambyo inaathiriwa katika uongezaji huo au ubadilishaji ni fonimu /f/. Hali hii imekuwa ni tofauti na lahaja ya Kitumbatu ambayo haina tabia ya kuongeza viyeyusho katika fonimu au kubadilisha viyeyusho hivyo ukilinganisha na muundo wa fonimu hizo katika Kiswahili Sanifu.

Mfano wa fonimu hizo ni:-

Fwana (Km) → fana (Kt) /fw/ → /f/

Kifwefwe (Km) → Kifyefye (Kt) /fw/ → /fj/

Kuwa na mbadala wa fonimu za irabu; lahaja ya Kimakunduchi na lahaja ya Kitumbatu imekuwa na tofauti katika matumizi ya irabu. Mfano;

Nyevu (Km) → Nivu (Kt) /e/ → /i/

Kidigi (Km) → Kidogo (Kt) /i/ → /o/

Vua (Km) → Vulya (Kt) /a/ → /ɪj/

Katika mifano ya hapo juu ni kuwa lahaja ya Kimakunduchi inatumia fonimu ya irabu /e/ ambayo ni tofauti na irabu /i/ inayotumika katika lahaja ya Kitumbatu, katika baadhi ya maneno. Pia inatumia irabu /i/ katika lahaja ya Kimakunduchi inatumika tofauti na lahaja ya Kitumbatu inayotumia irabu /o/ katika maneno “kidigi” na “kidogo”. Pia lahaja ya Kitumbatu inatumia fonimu ya /lj/ katika “vulya” wakati lahaja ya Kimakunduchi inatumia irabu ya /a/ katika neno “vua”.

4.5 Sababu za Kulingana na Kutofautiana kwa Lahaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu

Sehemu hii zimechambuliwa sababu za kulingana na kutofautiana kwa lahaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu kwa kutumia msingi wa nadharia ya Isimu Linganishi. Nadharia hii inaelekeza kuchambua data za lugha au lahaja zaidi ya moja ambazo zina asili moja ilikuona uhusiano wake wa kihistoria. Kutohana na hali hiyo, utafiti umebaini kuwa kufanana na kutofautiana kwa lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi kunatokana na sababu za kihistoria na uhusiano wa kijamii wa lahaja hizi. Kama ilivyochambuliwa hapo chini.

4.5.1 Sababu za Kulingana

Utafiti ulibaini kuwa zipo sababu kadha wa kadha ambazo zimesababisha kulinganaa kwa lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi. Miongoni mwa sababu hizo ni:-

4.5.1.1 Zinalingana Kwa sababu ya Kutoka Katika Asili ya Lugha Moja

Lahaja ya Kimakunduchi na lahaja ya Kitumbatu ni lahaja zinazotoka katika lugha asili moja ambayo ni lugha ya Kiswahili. Kipacha, (2003) anaeleza kuwa; jamii za wazungumza Kiswahili ziligawanyika katika makundi yaliyosemekana yametokana na

ama ukoo au matabaka. Kulikuwepo na wale ambao wametokana na maingiliano ya ndoa kati ya Waafrika na Waarabu ambao ni Watumbatu au Waafrika walioingiliana kindoa na Waajemi ambao leo hupendelea kijiita Washirizi, hao ni Wamakunduchi.

Lahaja zote zenye asili moja zinakuwa na msamiati wa msingi unaotoka katika lugha asili. Pia lahaja hizi zinakuwa na fonolojia yenye asili moja. Hivyo lahaja mbili hizi zimekuwa na fonimu zinazofanana kama ambavyo hufanana kwa baadhi ya msamiati na miundo ya tungo zake. Lahaja zote hizi zimekuwa na fonimu za msingi kutoka katika lugha ya Kiswahili. Matamshi yake yamekuwa na athari kubwa ya matamshi ya lugha ya Kiswahili. Na ndio maana wataalamu wa isimu ya Kiswahili wakakubaliana kuwa lahaja hizi ni miongoni mwa lahaja za lugha ya Kiswahili kutokana na kufanana kwa vipengele vya kiisimu.

4.5.1.2 Kuwa katika Kundi (Kanda) Moja ya Lahaja za Kiswahili

Lahaja ya Kimakunduchi na lahaja ya Kitumbatu zote hizi zimebekwa katika kanda moja za lahaja za kusini. Mgawo huu unatokana mgawo wa, Ahmed Kipacha (2003), katika uchambuzi wa lahaja amezigawa lahaja katika kanda mbili, ambazo ni kanda ya kusini na kanda ya kaskazini. Lahaja za kundi moja huwa na sifa na mambo yanayofanana kwa lahaja za kundi lote. Sifa hizi zaidi zimejikita katika isimu, kama vile fonolojia, mofolojia na hata sintakisia ya lahaja hizo. Hivyo lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi zipo katika kundi moja la lahaja kutokana na kuwa na sifa za msingi za kiisimu ambazo zinafafana. Zikiwemo sifa za kifonolojia. Ukweli huu umedhihirika kutokana na uchambuzi wa data za utafafiti huu, kama ilivyooneshwaa katika jedwali namba moja hapo juu.

4.5.1.3 Kufanana kwa Nyanja za Kiuchumi na Kiutamaduni/Kijiografia

Lahaja hizi zimekuwa na uwiano mkubwa na kufanana katika hali ya kijografia. Kipacha, (2003) anaeleza kuwa lahaja huweza kutokea kuwepo kwa sababu za kuhamahama zinazoweza sababisha wazungumzaji wa lugha kuhama kutoka sehemu moja kwenda nyingine na huku wakibeba lahaja na kuzitumia katika mazingira mapya. Data za utafiti huu zinadhahirisha kuwa watu wa jamii mbili hizi walianzia Tumbatu baadae kuhama na kuhamia eneo la Ng'anani, Makunduchi. Pia, jografia ya Tumbatu na Makunduchi ni sehemu kubwa ya ardhi yake ni ya mawe na zimepakana na bahari. Hali hizi zinasababisha wakaazi wake kujishughulisha na kilimo cha maweni pamoja na uvuvi. Kutokana na hali hizi wamekuwa na mfanano mkubwa wa misamiati inayotokana na uvuvi na kilimo cha maweni. Hivyo hata fonimu na matamshi yake yamekuwa yakifafana kwa asilimia kubwa. Mfano maneno kama “Kongwa na tumbaawe”. Katika neno “Kongwa” lenye maana ya baharini ambapo nyama kama kombe na kome wanaishi kwa wingi, fonimu /k/ katika lahaja zote wanaitamka kama ni /k^h/ ya mpumuo. Pia, fonimu /a/ katika neno tumbaawe inatamkwa katika mfumo wa fonimu /l^w/ au /l^r. Matamshi haya yanadhahirisha kufanana kwa lahaja hizi kutokana na misamiati ya baharini. Pia jamii hizi zimekuwa na mfanano katika masuala ya kiutamaduni. Jamii ya Makunduchi na jamii ya Tumbatu zote zimekuwa na utamaduni wa kutambika, mambo ya pungwa na koga mwaka. Utamaduni huu umekuwa na msamiati maalumu na kufanana katika matamshi ya fonimu zake kwa lahaja zote hizi mbili. Mfano katika sentensi ya “Taire mganga mkuru mungu” lahaja hizi katika mazingira ya uganga hutumia sentensi hii, na wanatumia “mkuru” badala ya neno la Kiswahili sanifu “Mkuu”. Hivyo fonimu /r/ katika neno hili inatumika katika lahaja zote hizi mbili.

4.5.2 Sababu za Kutofautiana

Lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakuduchi ni lahaja zilizotofautiana sana, kama ilivyochambuliwa hapo juu katika jadweli namba mbili. Kwa kuzingatia misingi ya Isimulinganishi lahaja mbili tofauti zenyenye asili moja huweza kufanana na kutofautiana kupitia msamiati wa msingi. Hivyo utafiti ulibaini kuwa lahaja hizi zinatofautiana katika kipengele hiki cha kifonolojia. Miongoni mwa tofauti hizi ni:

4.5.2.1 Umbali wa Kijiografia

Lahaja ya Kitumbatu ni lahaja inayozungumzwa katika kisiwa cha Tumbatu na eneo la Kaskazini mwa kisiwa cha Unguja. Kama vile Nungwi, Kidoti, Mkwajuni, Chaani, Matemwe kwengineko. Kipacha, (2003) anaeleza kuwa Lahaja ya Kitumbatu ni kisiwa kilichokuwepo Kaskazini Magharibi ya kisiwa cha Unguja karibu ya ghuba ya Mkokotoni. Kisiwa hiki ni sehemu ya wilaya ya Kaskazini ya Zanzibar. Wilaya hii ndio inayojulikana kuwa inazungumza lahaja ya Kitumbatu. Wakati lahaja ya Kimakunduchi inazungumzwa katika eneo la Makunduchi na eneo la Kusini mwa kisiwa cha Unguja. Umbali wa Kijiografia umesababisha kutofautiana kwa misamiati na matamshi ya fonimu zake katika lahaja hizi. Mfano ukirudi katika jedwali namba mbili unapata matamshi fonimu “ch” ya Kimakunduchi badala ya ile “s” ya lahaja ya Kitumbatu katika neno “chasoma” (Km) na “sasoma” (Kt).

Pia, jamii hizi zimetofautiana katika jiografia za ardhi zao. Jamii ya Makunduchi ina ardhi kubwa ambayo ipo katika hali ya mawe, hali ambayo inawafanya wanajamii wa jamii hii hasa wanaume kutokujishughulisha na kilimo. Jamii ya Tumbatu hasa katika maeneo yaliyo nje ya Kisiwa cha Tumbatu ni maeneo ya udongo ambayo yanarutuba

nzuri kwa kilimo. Hali ambayo inawafanya wanaume wengi wa jamii hii kujishughulisha na harakati za kilimo.

4.5.2.2 Maingiliano ya Kijamii

Lahaja hizi zimekuwa na maingiliano katika hali tofauti, suala ambalo limesababisha kutofautiana kwa misamiati. Kihistoria lahaja ya Kimakunduchi ni lahaja iliyokuwa na maingiliano ya hali ya juu. Jamii ya Makunduchi ni mionganoni mwa jamii iliyokuwa na mchanganyiko wa watu kutoka Bagamoyo, na sehemu nyingine za bara ya Tanzania Bara. Hali hii ilisababisha lahaja hii kuathrika zaidi kimatamshi na hata kimsamiati. Mionganoni mwa misamiati iliyoathirika na muingiliano huo misamiati yenye sauti “l” na “r” kama vile “Kula, lala” na mengineyo. Hali hii imekuwa ni tofauti kwa upande wa lahaja ya Kitumbatu. Kihistoria jamii ya Tumbatu ni jamii ambayo ilikuwa haina muingiliano mkubwa na watu kutoka nje ya Zanzibar na hata ndani ya Zanzibar yenewe. Hali hii ilisababisha lahaja hii kutokuathiriwa na matamshi ya lugha au lahaja zilizonje ya Zanzibar. Hata kama, hali hii imekuwa ikibadilika siku hadi siku, kwa sababu jamii hii imekuwa ikipokea wageni kutoka sehemu mbali mbali na kuifanya lahaja yake kubadilika hatua kwa hatua.

4.5.2.3 Kuathiriwa zaidi na Kiswahili Sanifu

Sababu nyingine ya kutofautiana kwa lahaja hizi ni kutokana na athari inayotokana na kuathiriwa na maendeleo ya Kiswahili sanifu. Kiwango cha athari katika lahaja hizi kinaonekana ni chenye kutofautiana. Kutokana na data zilizokusanywa katika utafiti hii, zinaonyesha kuwa lahaja ya Kitumbatu imeathiriwa zaidi na Kiswahili sanifu ukilinganisha na lahaja ya Kimakunduchi. Hali hii inatokana na ukweli kuwa katika fonimu za misamiati 18 iliyochambuliwa fonimu kumi na tatu (13) za Kitumbatu

zimefanana moja kwa moja na fonimu za Kiswahili Sanifu ambayo ni sawa na asilimia 72.22% ya kufanana. Na fonimu katika misamiati 2 ya Kimakunduchi ndiyo iliyofanana moja kwa moja na misamiati ya Kiswahili sanifu ambayo ni sawa na asilimia 11.11%. Kutokana na data hizo ni dhahiri kuwa lahaja ya Kitumbatu imeathiriwa zaidi na Kiswahili sanifu ukilinganisha la Lahaja ya Kimakundichi. Hii ni miongoni mwa sababu ya lahaja hizi kutofautiana kifonolojia.

4.5.2.5 Kiwango cha Jamii Kuathiriwa na Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia

Maendeleo ya sayansi na teknolijia nayo yamechukua nafasi kubwa katika kubadilisha na kuendeleza lahaja na lugha kwa ujumla. Tofauti ya kimaendeleo kutoka lahaja moja kwenda nyingine ni tofauti ambayo imeweza kuibua tofauti ya kimatamshi katika lahaja hizo. Jamii ya Tumbatu imekuwa na kiwango tofauti cha maendeleo katika nyanja ya Sayansi na Teknoloji ukilinganisha na jamii ya Makunduchi. Si rahisi kusema ni jamii ipi ipo juu zaidi katika maendeleo leo ya Sayansi na Teknolijia ila utafiti umebaini unaweza kuegemea katika kiwango cha lugha kuathiriwa zaidi kimatamshi kwa kuwa na misamiati ya kisayansi na kiteknolojia. Jedwali namba mbili linadhahirisha kuwa lahaja ya Kitumbatu ina kiwango kikubwa zaidi cha kuathirika na kuonesha kuwa huenda imeathiriwa na sayansi na Teknolojia.

Miongoni mwa tofauti hizo ni lahaja ya Kitumbatu inatumia neno “**vera**” lenye maana ya boti ya kusafirishia mizigo, “**tafya**” lenya maana kiungo ndani ya mwili wa kiumbe anachotumia kuvutia pumzi. “**Zepuleni**” kwa maana ya ndege, na “**figili**” kwa maana ya kifaa cha mziki cha taarabu (Udi). Hii inamaana kuwa lahaja ya Kitumbatu ipo katika hatua kubwa ya kisayansi kulinganisha na lahaja ya Kimakunduchi.

4.6 Hitimisho

Sura hii imejadili kwa kina malengo ya utafiti huu. Malengo mahsusi yamechambuliwa kwa lengo la kufikisha lengo la utafiti ambalo ni kuchunguza kufanana na kutofautiana kifonolojia katia ya lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi. Sura hii imegawanywa katika sehemu kuu nne. Kwanza dhana ya fonolojia; katika tasnifu hii imejumuisha kuwa, fonolojia ni taaluma inayoshughulika na uchambuzi wa sauti zinazotumika katika lugha maalumu kwa kuangalia ala za sauti, namna zinavyotamkwa na sifa zake. Tasnifu hii katika kuchambua tawi hili la isimu ilijikita katika kuchambua fonimu na matamshi yake. Fonimu ndio kipashio cha msingi cha fonolojia ya lugha.

Pili, kazi hii imeeleza juu ya mlingano wa fonimu na matamshi yake katika lahaja ya Kimakunduchi na lahaja ya Kitumbatu. Katika kipengele hiki, utafiti ulijikita katika uchambuzi wa fonolojia kwa kuangalia fonimu za msamiati na namna zinavyotamkwa. Fonimu za misamiati hamsini zimechambuliwa na kupata misamiati kumi na tano (15) ambazo fonimu zake zinalingana (kama ilivyobainishwa katika jedwali namba tatu) na kubainika kuwa lahaja hizi zinafanana katika vipengele vifuatavyo: kuwa na silabi zenyе sifa ya kudondosha fonimu, usilimisho wa fonimu na kuimarisha na kudhofisha fonimu.

Tatu, Tofauti za fonimu kati ya lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi imechambuliwa kwa kina. Katika kuchambua tofauti za fonimu katika lahaja hizi misamiati hamsini (50) imechambuliwa na misamiati kumi na nane (18) imeonesha tofauti ya fonimu hizo. Kama ilivyooneshwa katika jedwali namba nne. Vipengele vilivyojenga tofauti ya kimatamshi katika lahaja hizi ni: ukakaishaji wa fonimu,

kuimaraika na kudhoofika kwa matamshi ya fonimu, uyeyushaji wa fonimu pamoja na tofauti nyingine ambazo ni fonimu /v/ ya Kimakunduchi inayokaa badala ya fonimu /p/ ya Kitumbatu, na fonimu nyingine nyinginez.

Mwisho ilikuwa ni mjadala wa sababu za kufanana na kutofautiana kwa matamshi ya fonimu za lahaja hizo. Sababu za kufanana kwa lahaja hizi ni: zote hizi ni lahaja zenye asili moja, zote hizi zipo katika kundi moja la lahaja kwa mujibu wa mgawanyo wa Kipacha (2003) pamoja na kuwa lahaja zote hizi kuwa na nyanja za aina moja za kiuchumi. Kwa upande wa sababu za kutofautiana ni: umbali wa Kijiografia kwa maeneo yanayozungumzwa lahaja hizi, maingiliano ya kijamii katika lahaja hizi, kuathiriwa na Kiswahili sanifu, uwezo wa hali ya kiuchumi kwa wanajamii wa lahaja hizi na kiwango cha jamii kuathiriwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

SURA YA TANO

MUHUTASARI WA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumetoa hitimisho kuhusu utafiti wetu. Sura yenyewe ina sehemu tatu. Sehemu ya kwanza imebeba muhtasari wa tasnifu hii kwa jumla; ya pili imezungumzia mchango au mambo mapya ambayo yameibuliwa na utafiti huu. Na mwisho ni hitimisho la sura hii na pia ni hitimisho la kazi hii kwa jumla.

5.2 Muhutasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita kuchunguza ulinganishi wa kifonolojia kati ya lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi, ambapo vipengele vinavyotoa mlingano na mtofautiano wa matamshi ya fonimu za lahaja hizi vilibainishwa na kujadiliwa. Maeneo yaliyotafitiwa ni kisiwa cha Tumbatu kwa lengo la kupata matamshi ya fonimu za lahaja ya Kitumbatu na shehia za Makunduchi kwa ajili ya kupata matamshi ya fonimu za lahaja ya Kimakunduchi. Utafiti ulilenga mambo matatu yafuatayo: Kuchambua mlingano wa matamshi ya fonimu uliopo kati ya lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi. Kuchambua tofauti za matamshi ya fonimu yaliyopo kati ya lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi. Na, kuelezea sababu zilizosababisha kulingana na kutofautiana kwa matamshi ya fonimu ya Kitumbatu na Kimakunduchi. Matokeo ya tasnifu hii yamekuwa na mchango mkubwa kwa taaluma ya lahaja na lahajia pamoja na isimu ya Kiswahili kwa jumla. Ni dhahiri kuwa wasomi na wataalamu wa lahaja na isimu wataitumia vilivyo kazi hii kama ni rejelea ya kitaaluma. Mionganini mwa michango iliyojipambanua katika kazi hii ni:

Kubainisha msamiati wenyе maumbo na maana sawа kutoka lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi. Msamiati huu umechambuliwa mlingano na kutofautiana kwake katika kiwango cha matamshi ya fonimu zake. Suala hii ni muhimu kwa watafiti na wanafunzi wa lahaja katika kujua uhusiano wa lahaja hizi kifonolojia pamoja na kuona mwachano wake katika kipengele hicho cha kifonolojia.

Mchango wa pili ni kubainisha na kuchambua vipengele vinavyojenga mlingano wa matamshi ya fonimu kwa lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi. Utafiti umebaini kuwa lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi yamekuwa na fonimu za kipekee kulinganisha na Kiswahili sanifu, pia zipo zimekuwa na matamshi ambayo ni tofauti na matamshi ya fonimu katika Kiswahili sanifu. Uchambuzi huu utakuwa ni msada kwa wanaisimu kwa kujenga uhisiano wa kiasili kwa lahaja hizi na kuizilinganisha na lahaja nyingine za Kiswahili.

Mchango wa tatu ni kubainisha na kuchambua vipengele vinavyojenga tofauti ya matamshi ya fonimu za lahaja ya Kimakunduchi na lahaja ya Kitumbatu. Watu wengi wemekuwa wakiamini kuwa lahaja ya Kimakunduchi na lahaja za Kitumbatu ni lahaja moja zenye matamshi ya aina moja. Utafiti huu utasaidia kupambanua tofauti ya matamshi haya, kwa kuangalia vipengele vinavyojenga tofauti za kimatamshi katika lahaja hizi.

Mchango mwingine ni kuchambua sababu za kulingana na kutofautiana kwa matamshi wa lahaja hizi. Ni dhahiri kuwa sababu za kulingana na kutofautiana kwa matamshi ya fonimu za lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi ni sababu zile zile zinazosabaisha kuibuka kwa lahaja katika lugha fulani. Kazi hii imechangia

kuthibitisha juu ya sababu za kuibuka kwa lahaja katika lugha kutokana na kuwa ni sababu za msingi za kulingana na kutofautiana kwa lahaja za lugha.

Tasnifu hii ina jumla ya sura tano. Sura ya kwanza ni sura inayotambulisha tatizo la utafiti. Utambulisho umeanza kwa kueleza historia fupi ya lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi. Pia, usuli wa tatizo umeleza juu ya dhana na mitazamo mbali mbali kuhusu lahaja za Kiswahili. Vile vile, imeeleza tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti na manufaa ya utafiti.

5.3 Mapendekezo ya Tasnifu hii

Utafiti huu ulitoa mapendekezo ya aina mbili; mapendekezo ya jumla juu ya maendeleo na mustakibali wa lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi.

5.3.1 Mambo Yakuboreshwa Zaidi Katika Lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi

Kutokana na mchakato wa kazi hii utafiti umeweza kubaini maoni yafutayo: Mosi, utafiti ulibaini kuwa katika lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi kuna fonimu katika baadhi ya misamiati yake ambazo bado hazijapatiwa tahajia zake. Hivyo imekuwa vigumu kuandika maneno hayo kwa uhalisi kama wenyiji wa lahaja hizi wanavyotamka. Hivyo ni vyema kwa wanaisimu waliobobea katika masuala ya kifonolojia kuliangalia suala hili kwa kina na kulifanyia kazi. Mfano wa fonimu hizo ni fonimu /l/ katika maneno “lala” na “kula”. Maneno haya yamekuwa hayana tahajia halisi kama yanavyotamkwa katika lahaja ya Kitumbatu na hasa matamshi ya wanajamii wa kisiwa cha Tumbatu. Utafiti ulibainisha kuwa fonimu /l/ katika maneno haya mawili katika lahaja hii yanachukua fonimu mbili tofauti.

Pili, taasisi za kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili kuona haja ya kuandika Kamusi Kuu la Lahaja za Kiswahili. Suala hili litasaidia jamii na wanafunzi wa lugha ya Kiswahili kujifunza lahaja hizi kwa urahisi na kuwaka kumbukumbu nzuri ya kuzitunza lahaja hizi. Lahaja hizi zimekuwa na mabadiliko makubwa kiasi cha kuwa na tofauti kubwa kati ya vijana na wazee ndani ya lahaja moja na kuonesha kuwa vijana wamekuwa wanapoteza lahaja zao kwa kasi kubwa kutohakana na maendeleo ya sayansi na teknolojia yanayowakumba vijana hawa.

Wataalamu na wanaisimu wa lugha ya Kiswahili kutafiti na kuchambua lahaja za Kiswahili. Ukweli ni kuwa bado marejeleo yanayohusiana na lahaja katika lugha ya Kiswahili bado ni machache na hivyo kufanya wanafunzi wanaosoma na kutafiti mambo ya lahaja kupata shida na hata kuvunjika moyo wa kutafiti masula ya lahaja na lahajia.

5.3.2 Mapendekezo ya Tafiti za Baadae

Tafiti nyingi zimefanywa juu ya lahaja za Kiswahili, ila kuna mambo mengi zaidi na ya msingi yanahitaji kufanyiwa utafiti katika lahaja hizi. Miongoni mwa machache ambayo tasnifu hii imegundua na kuona ipo haja ya kufanyiwa utafiti ni:

Kutafiti juu ya athari ya sayansi na teknolojia katika lahaja za Kiswahili. Utafiti huu utasaidia kuibua msamati wa asili na matamshi yake kwa lahaja hizi na mabadiliko yake kulinagana na mendeleo ya sayansi na teknolojia.

Kutafiti juu ya mabadiliko ya kifonolojia katika lahaja za Kiswahili. Kazi hii iligundua kuwa katika lahaja hizi kunakuwa na tofauti kubwa ya kifonolojia kutoka sehemu moja ya lahaja na nyingine. Hali hii inasababisha baadhi ya watu wakawaida

na hata wataalamu wa isimu kuamini kuwa ni lahaja mbili tofauti. Hali hiyo huweza kuthibitishwa kuitia hoja za kitaalamu zilizofanyiwa utafiti na sio maoni binafsi.

5.4 Hitimisho

Lahaja ya Kitumbatu na lahaja ya Kimakunduchi ni lahaja zilizolingana na pia kutofautiana katika baadhi ya matamshi ya fonimu za msamiati wake. Kulingana huku kunathibitisha kuwa ni lahaja zenye asili moja na zilizokuwa na ukaribu wa kijiografia kulinganisha na lahaja nyingine za Kiswahili. Pia kwa upande wa tofauti za kimatamshi katika fonimu zake zinazodhiihirisha kuwa ni lahaja mbili tofauti zenye kujitegemea. Hali hii inadhihirika kutokana na uchambuzi wa data zilizochambuliwa hapo juu. Jumla ya misamiati hamsini ilikushanywa na kuchambuliwa, misamiati ambayo msingi wake ni kutoka katika lugha ya Kiswahili. Pamoja na msamiati huu wa msingi, pia upo msamiati ambao unajitegemea kwa kila lahaja kama ilivyo katika jedwali namba 4.

MAREJELEO

- Allen, H. B. & Linn, M. D. (wah.) (1986). *Dialect and Language Variation*. New York: Academic Press Inc., Harcourt B.J. Publishers.
- Athumanji, M. R. (2015). Athari za Kiisimu za Luga ya Kiswahili katika Luga ya Kiyao. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (haijachapwa).
- Bakari, B. K. (2015), Ulinganishaji wa Kiisimu Kati ya Lahaja ya Kipemba na Kitumbatu. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri ya Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- BAKIZA, (2012). Kamusi la Lahaja ya Kimakunduchi. BAKIZA, Zanzibar.
- Bavuai, A. I. (2016). Muundo wa Kirai Nomino katika Lahaja ya Kimakunduchi. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Zanzibar, Tanzania. (Haijachapwa).
- Enon, C. J. (1995). *Educational Research, Statistics and Measurement*. Kampala: Department of Distance Education Institute of Adult and Continuing Education. Chuo Kikuu cha Makerere.
- Goldsmith, J. A. (1990). *Autosegmental and Metrical Phonology*. Great Britain: TJ Press Ltd.
- Habwe, J., and Karanja, P. (2004). *Msingi wa Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Haule, F. (2014). Muundo wa Njeo za Luga ya Kingoni. Tasnifu za Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta: Haijachapishwa.
- Hill, (1972). The primary Dailects of Swahili. Aproach to Lingustic and Geographical Survey in Swahili, vol &3/2 (pp-7-18) (Imepakuliwa 24/05/2017)

- Kahn, D. (1976). *Syllable – Based Generalization in English Phonology. PhD Dissertation.* MIT. Published by Garlan.
- Katamba, F. (1989). *An Introduction to Phonology.* New York: Longman Publishers.
- Kipacha, A. (2003). OSW 303 Lahaja za Kiswahili. Chuo Kikuu huria cha Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.
- Kombo, K. na Tromp, D. (2006). Propsal and Thesis Writing: Introduction. Nairobi: Paulines Publication Africa.
- Kothar C. R. (2009). *Research Methodology Methods and Techniques (Toleo la pili).* New Delhi: New Age International (P) Limited.
- Kothar, C. R. (2004). *Research Methodology Methods and Techniques (Toleo la pili).* Ne Delhi: New Age International (P) Limited.
- Kothar, C. R. (2009). *Reasearch methodology.* New Delhi: New Age International (P) Limited.
- Kress, T. M. (2008). *Critical Praxis Research, Breathing New Life into Research Methods for Teachers.* Washington, DC: Springer.
- Lambert, H. E. (1957). *Ki-Vumba: A Dialect of Mombasa Coast.* Kampala: East African Swahili Commettee.
- Lass, R. (1984) *Phonology. An Introduction to basic phonology.* Cambridge: Cambridge University Press.
- Maganga, C. (1991). A Study of Morphophonology of standard Kiswahili, Kipemba, Kitumbatu na Kimakunduchi. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Makame, M. A. (2016), Athari za Utandawazi Katika Lahaja ya Kitumbatu. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Haijachapishwa.

- Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*: Dar-es-Salaam. TUKI.
- Massamba, Kihore na Hokororo, (2001). Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA). Sekondari na Vyuo. TUKI, Dar es Salaam, Tanzania.
- Masebo, J. A. & Nyamwingine, N. (2002). Nadharia ya Lugha ya Kiswahili. Afroplus Industrial Ltd. Dar es Salaam, Tanzania
- Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha: Isimu na Nadharia*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.
- Mgullu, R. S. (1999). *Mtaala Wa Isimu. Fonetiki, Fonolojia na Mofonolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhom Publishers.
- Mkude, J. S. (1993). *Mtawanyiko wa Lahaja ya Kiswahili TUKI*. Makala za waandishi wa Kiswahili TUKI.
- Msanjila, Y. P. (2009). *Isimu Jamii: Sekondari na Vyuo*. Dar es salaam: TUKI.
- Ngowa, N. J. (2015). Uchanganuzi wa Nomino-Mkopo za Kigiriyama kutoka Kiingereza. Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu ya Chuo Kikuu cha Pwani (haijachapwa).
- Nurse, D. and Hinnebusch, T. (1993). *Swahili and Sabaki A linguistic History*. London, University of California.
- Nurse, D., and Speer, T. (1985). *The Swahili: Reconstructing the history and Language of an Africa society*. London: University of California.
- Oxford Advanced Learners Dictionary, (2000), *Oxford Advanced Learners Dictionary of Current English*. Nairobi: Oxford University Press
- Polome, E. C. (1967). *Swahili Language Hand book, Centre for Applied linguistics*. Washington, DC: Sage Publications Inc.

- Salehe, A. M. S. (2013). Athari za Kiisimu za Lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu Kinachotumika Shulenii Makunduchi, Zanzibar. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Zanzibar, Tanzania.
- Samsom, R. H. (1999). *Asein-Afrika-Institut Universitat Hamburg Institut fur Afrikanistik Universitat*. Leipzig: Universitat subbibliothek Publishers.
- TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Tunu za Kiswahili (2013a). *Lahaja za kijamii*: Retrieved on 24th March 2017 from> [[www.tunuza-kiswahili.blogspot.com /p/blog-page_6.html](http://www.tunuza-kiswahili.blogspot.com/p/blog-page_6.html)].
- Tunu za Kiswahili (2013b) *Fonolojia arudhi*: Retrieved on 24th March 2017 from: [[www.tunuza-kiswahili.blogspot.com /p/blog-page.html](http://www.tunuza-kiswahili.blogspot.com/p/blog-page.html)].
- Williman, N. (2011). *Research Methods.The Basic*, New York: Routage Taylor and Francis Group.

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho Na. 1: Muongozo wa Hojaji, Usaili na Ushuhudiaji

A: 1. MUONGOZO WA USAILI

Utafiti huu unahusiana na mada ya “Kulingana na kutofautiana kifonolojia kati ya Lahaja ya Kimakunduchi na Lahaja ya Kitumbatu”. Utafiti huu kwa ajili ya kuendeleza taaluma ya Kiswahili na hauna uhusiano wowote na masuala ya kisiasa. Unaombwa kujibu maswali haya kwa usahihi na kuzingatia kuwa taarifa utakazo towa zitatumika kwa lengo la utafiti huu tu, na hazitatumika kwa lengo jengine.

Jibu maswali yafuatayo kwa usahihi kadri uwezavyo;

1. Jee ni vipi/kwa vipengele gani lahaja ya Kitumbatu inafanana na kutofautiana na lahaja ya Kimakunduchi.
2. Ni sauti/matamshi yepi ya lahaja ya Kitumbatu yanafanana na ya Lahaja ya Kimakunduchi (Taja sauti/matamshi yanayofanana)
3. Ni sauti/matamshi yepi ya Lahaja ya Kimakunduchi yanatofautiana na ya lahaja ya Kitumbatu (Taja sauti/matamshi yanayotofautiana)
4. Kulingana na kutofautiana kwa sauti hizo huweza kuathiri maneno ya lahaja hizo kimaana
5. Eleza sababu zinazosababisha kutokea mlingano na mtarfautiano kwa lahaja hizo:
 - a) Kijamii (mahusiano na maingiliano ya kijamii)
 - b) Kiuchumi (shughuli za kiuchumi za kijamii)
 - c) Kisiasa (shughuli za kiutawala)

A: 2 MUONGOZO WA HOJAJI

Utafiti huu unahusiana na mada ya “Kulingana na kutofautiana kifonolojia kati ya Lahaja ya Kimakunduchi na Lahaja ya Kitumbatu”. Utafiti huu kwa ajili ya kuendeleza taaluma ya Kiswahili na hauna uhusiano wowote na masuala ya kisiasa. Unaombwa kujibu maswali haya kwa usahihi na kuzingatia kuwa taarifa utakazo towa zitatumika kwa lengo la utafiti huu tu, na hazitatumika kwa lengo jengine.

Jibu maswali yafuatayo kwa kuweka alama ya vyema au kama swali litakavyokuelekeza.

- Una miaka mingapi?

Miaka 20 – 29	
Miaka 30 – 39	
Miaka 40 – 49	
Miaka 50 na kuendelea	

- Ni ipi jinsi yako?

Mke	
mme	

- Unatumia lahaja gani?

Kimakunduchi	
Kitumbatu	

- Jee ni vipi/kwa vipengele gani lahaja ya Kitumbatu inafanana na kutofautiana na lahaja ya Kimakunduchi

.....

.....

.....

.....

5. Taja sauti/matamshi ya lahaja ya Kitumbatu yanayofanana na ya Lahaja ya Kimakunduchi

.....
.....
.....
.....

6. Taja sauti/matamshi yepi ya Lahaja ya Kimakunduchi yanatofautiana na ya lahaja ya Kitumbatu

.....
.....
.....
.....
.....

7. Eleza kwa vipi kulingana na kutofautiana kwa sauti hizo kumeweza kuathiri maneno ya lahaja hizo:

- a) Kimaana

.....
.....

- b) Kisintaksia (katika muundo wa sentensi)

.....
.....
.....

- c) Kimofolojia (katika muundo wa maneno)

.....
.....
.....
.....

8. Eleza sababu zinazosababisha kutokea mlingano na mtofautiano kwa lajaja hizo:

d) Kijamii (mahusiano na maingiliano ya kijamii)

.....
.....
.....
.....

e) Kiuchumi (shughuli za kiuchumi za kijamii)

.....
.....
.....
.....

f) Kisiasa (shughuli za kiutawala)

.....
.....
.....
.....

9. Eleza mazingira ya kifonolojia ya kutofautiana kwa sauti za lajaja mbili hizi

.....
.....
.....
.....

10. Katika sauti zilizotofautiana katika lajaja hizi (Kimakunduchi na Kitumbatu) ni
ipi sauti iliyoathirika na ipi sauti ya asili

.....
.....
.....

A: 3 MUONGOZO WA USHUHUDIAJI

1. Mtafiti atatafuta mwenyeji wa katika maeneo yanayozungumzwa lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi.
2. Mtafiti atakwenda maeneo husika kwa kufuata ratiba za kiutawala wa maeneo na maadili ya kiutafiti.
3. Mtafiti atazungumza na wazee wa maeneo ya Tumbatu na Makunduchi kwa lengo la kufanya uchunguzi makini juu ya:
 - a) Namna wanavyotamka maneno ya lahaja husika
 - b) Kuangalia mazingira halisi ya watumiaji wa lahaja kiuchumi, kisiasa na kijamii.
 - c) Kulinganisha na kutofautisha matamshi hayo kutoka lahaja moja na nyingine.
4. Mtafiti atarikodi na kuchukua picha juu ya matukio hayo kwa kuzingatia maadili ya utafiti.
5. Mtafiti atatoa shukrani na kurudi kwa lengo la kuendelea na shughuli nyingine za kiutafiti.

Kiambatanisho Na. 2: Matukio Mbalimbali ya Kiutafiti Kupitia Picha



Pichani ni Mtafiti (kulia) akihojiana na mzee bi (Mwanajuma Ndundu) kutoka Makunduchi kuhusu lahaja ya Kimakunduchi. (Chanzo ni Mtafiti)



Mtafiti (kushoto) akiwa na Mtafitwa kutoka katika jamii ya Makunduchi bi (Nyausi Haji) na kuonesha hali halisi ya mazingira ya Makunduchi.



Mtafiti (kushoto) akiwa anahojiana na mzee (Mzee Issa Ali) kutoka Makunduchi kuhusiana na lahaja ya Kimakunduchi.



Mtafiti (kushoto) akimuhoji mmoja kati ya wazee wa Makunduchi(Pandu Muombwa) kuhusiana na lahaja ya Kimakunduchi.



Hii ni picha inayooonesha sura halisi ya mazingira ya kisiwa cha Tumbatu. Picha iyopigwa na mtafiti akiwa ndani ya chombo wakita akitaka kushuka na kuingia ndani ya kisiwa cha Tumbatu.